JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

JANUARI, 2016

YALIYOMO

UTANGULIZI ----------iii

SURA YA KWANZA ----------1
HALI YA UCHUMI----------1
1.1 Uchumi wa Dunia----------1
1.2 Uchumi wa Taifa----------1
1.2.1 Ukuaji wa Pato la Taifa ----------1
1.2.2 Idadi ya Watu na Pato la Kila Mtu----------3
1.2.3 Viashiria vya Umasikini ----------3
1.2.4 Mfumuko wa Bei----------3
1.2.5 Ujazi wa Fedha na Karadha ----------4
1.2.6 Mwenendo wa Viwango vya Riba----------4
1.2.7 Thamani ya Shilingi ----------5
1.2.8 Urari wa Biashara----------5
1.2.9 Akiba ya Fedha za Kigeni ----------6
1.2.10 Mapato na Matumizi ya Serikali----------6
1.2.11 Deni la Taifa ----------7

SURA YA PILI ----------8
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO ----------8
2.1 Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/15 ----------8
2.1.1 Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa ----------8
2.1.2 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati----------9
2.2 Ushiriki wa Sekta Binafsi----------22
2.3 Changamoto na Hatua za Kukabiliana----------23

SURA YA TATU ----------24
VIPAUMBELE VYA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17----------24
3.1 Malengo----------24
3.2 Vipaumbele ----------24
3.2.1 Viwanda vya Kuimarisha kasi ya Ukuaji wa Uchumi ---------- 24
3.2.2 Miradi Mikubwa ya Kielelezo (flagship projects)---------- 25
3.2.3 Maeneo Wezeshi kwa Maendeleo ya Viwanda---------- 25
3.2.4 Kufungamanisha Maendeleo ya Viwanda na Malengo ya Maendeleo ya Watu---------- 30

3.2.5 Maeneo Mengine Muhimu kwa ukuaji wa Uchumi na Ustawi wa Taifa ---------- 33

SURA YA NNE ---------- 35
UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17 ---------- 35
4.1 Utangulizi ---------- 35
4.2 Ugharamiaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) ---------- 35
4.3 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2015/16 ---------- 36
4.4 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2016/17 ---------- 36
4.5 Vyanzo vya Mapato ya Ndani ---------- 37
4.6 Vyanzo vya Mapato ya Nje ---------- 37
4.7 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ---------- 37
4.8 Uwekezaji wa Sekta Binafsi ---------- 38

SURA YA TANO ---------- 39
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ---------- 39
5.1 Utangulizi ---------- 39
5.2 Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo ---------- 39
5.2.1 Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa ---------- 39
5.2.2 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati ---------- 39
5.2.3 Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa ---------- 47
5.3 Mgawanyo wa Majukumu ---------- 48

SURA YA SITA ---------- 50
VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO ---------- 50
6.1 Utangulizi ---------- 50
6.2 Vihatarishi katika kutekeleza Mpango ---------- 50
6.3 Mikakati ya Kukabiliana na Vihatarishi ---------- 51

Kiambatisho I: Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 2014/15 ---------- 53

Kiambatisho II: Ratiba ya Uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2016/17 ---------- 80

UTANGULIZI

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 yanalenga kutekeleza Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 – 2025/26) na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mapendekezo haya ni msingi wa kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 unakusudiwa kuwa na maeneo ya vipaumbele vinne:- viwanda vya kuimarisha kasi ya ukuaji wa uchumi; miradi mikubwa ya kielelezo ya kuwezesha uchumi kupaa (flagship projects); miradi inayoendelea, hususan ya maeneo wezeshi (barabara, reli, bandari, maji na mawasiliano) kwa maendeleo ya viwanda; na maeneo yatakayolenga kufungamanisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu. Lengo kuu la Mpango huu ni kuhakikisha kuwa rasilimali na fursa za nchi zinatumika vizuri ili kujenga uchumi wa viwanda na kupunguza umaskini. Ili kufikia malengo hayo, mikakati itakayotumika ni pamoja na: kuanza na viwanda vilivyopo na kuhakikisha vinafanya kazi, hususan, viwanda vilivyobinafsishwa kwa wawekezaji binafsi kwa makubaliano ya kuviendeleza; kuhimiza na kushawishi wawekezaji kuwekeza katika maeneo mbalimbali nchini; na kuondoa vikwazo kwa kuimarisha mazingira ya kufanya biashara.

Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 yamezingatia: dhamira ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ya kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati; Mpango Elekezi wa Miaka Kumi na Tano (2011/12 – 2025/26); maamuzi ya Serikali ya kuunganisha mfumo wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania Awamu ya Pili (MKUKUTA II) katika mfumo mmoja jumuishi; na taarifa ya awali ya maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Pia, yamezingatia sera na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya kisekta, kikanda (EAC na SADC) na Umoja wa Afrika; Malengo ya Maendeleo Endelevu, 2030; Ilani ya CCM ya uchaguzi wa mwaka 2015; na hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wakati akifungua rasmi Bunge la 11 yenye msisitizo wa ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 kimegawanyika katika sura kuu sita. Sura ya kwanza ni hali ya

uchumi wa Dunia na Taifa. Sura ya pili ni mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/15 na nusu ya mwaka 2015/16. Sura ya tatu ni maeneo ya vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17. Sura ya nne ni ugharamiaji wa mpango wa maendeleo. Sura ya tano inaainisha ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo. Sura ya sita ni mkakati wa kukabiliana na vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango.

SURA YA KWANZA

HALI YA UCHUMI

1.1 Uchumi wa Dunia

Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya Oktoba 2015, inaonesha kuwa kwa kipindi cha mwaka 2013 na 2014, Pato la Dunia lilikua kwa wastani wa asilimia 3.3 na asilimia 3.4 kwa mtiririko huo. Ukuaji huo ulichangiwa na: kuongezeka kwa ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea kutoka asilimia 1.1 mwaka 2013 hadi asilimia 1.8 mwaka 2014; kushuka kwa bei za nishati ya mafuta katika soko la Dunia na hivyo kuchangia kushuka kwa gharama za uzalishaji; na kuongezeka kwa mahitaji ya kiuchumi katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea. Ukuaji katika nchi zilizoendelea ulichangiwa kwa kiwango kikubwa na sera imara za fedha na matumizi; kushuka kwa bei za nishati katika soko la Dunia; na ukuaji wa sekta ya fedha na mikopo. Aidha, matarajio ya ukuaji wa Pato la Dunia ni kukua kwa wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2015 na asilimia 3.6 mwaka 2016. **Jedwali Na. 1.1** linaonesha mwenendo wa ukuaji wa pato la dunia kuanzia mwaka 2008 hadi 2014 na matarajio ya mwaka 2015 na 2016.

Jedwali 1.1: Ukuaji wa Pato la Dunia (2008-2014) na Matarajio (2015 – 2016)

	Halisi (Asilimia)							Matarajio (Asilimia)	
	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Dunia	3.1	0.0	5.4	4.2	3.4	3.3	3.4	3.1	3.6
Nchi Zilizoendelea	0.2	-3.4	3.1	1.7	1.2	1.1	1.8	2.0	2.2
Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea	5.8	3.1	7.4	6.2	5.2	5.0	4.6	4.0	4.5
Nchi Zinazoibukia Barani Asia	7.3	7.5	9.6	7.7	6.8	7.0	6.8	6.5	6.4
Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara	6.0	4.0	6.7	5.0	4.2	5.2	5.0	3.8	4.3
Tanzania	5.6	5.4	6.4	7.9	5.1	7.3	7.0	6.9	7.0
Kenya	0.2	3.3	8.4	6.1	4.5	5.7	5.3	6.5	6.8
Uganda	10.4	8.1	7.7	6.8	2.6	3.9	4.8	5.2	5.5
Rwanda	11.2	6.2	6.3	7.5	8.8	4.7	7.0	7.0	7.0
Burundi	4.9	3.8	5.1	4.2	4.0	4.5	4.7	4.8	5.0

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa, Oktoba 2015

1.2 Uchumi wa Taifa

1.2.1 Ukuaji wa Pato la Taifa

Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2014 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.3 mwaka 2013. Takwimu hizi zimezingatia marekebisho ya mwaka wa kizio yaliyofanyika mwaka 2014 kwa kutumia mwaka wa kizio 2007 badala ya mwaka 2001. Marekebisho haya

yameleta mabadiliko katika Pato la Taifa na michango ya sekta mbalimbali kwenye Pato la Taifa. Ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa mwaka 2014 unaonesha kuwa sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni pamoja na: ujenzi (asilimia 14.1); usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 12.5); fedha na bima (asilimia 10.8); na biashara na matengenezo (asilimia 10.0). Aidha, sekta ya kilimo (mazao, ufugaji, misitu na uvuvi) ambayo inaajiri idadi kubwa ya wananchi ilikua kwa kasi ndogo ya asilimia 3.4. Sekta ya kilimo bado inatoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa wa asilimia 28.9. Ukuaji wa uchumi kwa kipindi cha robo ya tatu (Julai hadi Septemba) ya mwaka 2015 ulikuwa asilimia 6.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na ukuaji kwenye sekta za ujenzi, usafirishaji na uhifadhi wa migizo, huduma za utawala, mawasiliano na huduma za fedha na bima. **Jedwali Na. 1.2** linaonesha mwenendo wa ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi katika kipindi cha mwaka 2009 hadi 2014.

Jedwali 1.2: Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi 2009 hadi 2014 (kwa bei za mwaka 2007)

Shughuli za Kiuchumi	Ukuaji (Asilimia)					
	2009	**2010**	**2011**	**2012**	**2013**	**2014**
Kilimo, Misitu na Uvuvi	5.1	2.7	3.5	3.2	3.2	3.4
• Mazao	5.5	3.7	4.8	4.2	3.5	4.0
• Mifugo	5.3	1.4	1.6	1.8	2.0	2.2
• Uwindaji na Misitu	5.1	3.4	3.3	3.5	4.7	5.1
• Uvuvi	0.5	0.9	2.6	2.9	5.5	2.0
Viwanda	4.7	8.9	6.9	4.1	6.5	6.8
Umeme	4.3	13.4	-4.3	3.3	13.0	9.3
Maji Safi na Majitaka	4.6	2.2	-1.2	2.8	2.7	3.7
Ujenzi	-3.8	10.3	22.9	3.2	14.6	14.1
Biashara na Matengenezo	2.7	10.0	11.3	3.8	4.5	10.0
Usafirishaji na Uhifadhi Mizigo	6.9	10.7	4.4	4.2	12.2	12.5
Malazi	1.0	3.7	4.1	6.7	2.8	2.2
Mawasiliano	26.6	24.4	8.6	22.2	13.3	8.0
Fedha na Bima	18.4	12.6	14.8	5.1	6.2	10.8
Upangishaji Nyumba	1.8	1.8	1.9	2.0	2.1	2.2
Shughuli za Kitaaluma, Sayansi na Ufundi	15.8	29.9	4.8	-5.8	5.4	0.5
Huduma Zinazohusiana na Utawala	0.4	8.6	5.1	23.8	12.2	6.0
Utawala na Ulinzi	-0.7	-5.0	15.9	9.1	7.8	3.9
Elimu	9.2	6.4	5.6	7.4	4.3	4.8
Afya na Ustawi wa Jamii	7.4	3.3	5.3	11.4	8.8	8.1
Sanaa na Burudani	3.0	7.3	7.7	11.0	5.7	5.7
Huduma Nyingine za Kijamii	5.9	6.0	6.2	6.4	6.5	6.7
Shughuli za Kaya Binafsi Katika Kuajiri	2.7	2.7	2.7	2.7	2.7	2.7
Pato la Taifa	**5.4**	**6.4**	**7.9**	**5.1**	**7.3**	**7.0**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2015

1.2.2 Idadi ya Watu na Pato la Kila Mtu

Tanzania ilikadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 46.1 na Pato la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 79.44 katika mwaka 2014. Aidha, wastani wa Pato la kila mtu lilikuwa shilingi 1,724,416 (dola za Kimarekani 1,043) mwaka 2014 ikilinganishwa na shilingi 1,582,797 (dola za Kimarekani 948) mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 8.9. Kiwango hiki kinaiweka Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazokaribia kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kipato cha kati ambacho ni dola za Kimarekani 1,046 – 12,745. Kwa msingi huo, ni dhahiri kuwa bado kunahitajika msukumo zaidi wa kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa ili kufikia malengo ya Dira ya Dola za Kimarekani 3,000 na nchi ya uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

1.2.3 Viashiria vya Umasikini

Tafiti za mapato na matumizi katika kaya, zinaonesha kuwa kiwango cha umasikini mijini na vijijini kimepungua. Mwenendo huu unaashiria kuwa kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi ya wastani wa asilimia 6.5 kwa mwaka iliyofikiwa katika kipindi cha muongo mmoja na nusu uliopita imeanza kuwanufaisha wananchi wengi. Umasikini ulipungua kutoka asilimia 39 mwaka 1992 hadi asilimia 34.4 mwaka 2007 sawa na asilimia 4.6 kwa kipindi cha miaka 15. Katika kipindi cha miaka 5 iliyopita umasikini umepungua kwa asilimia 6.2 kutoka asilimia 34.4 mwaka 2007 hadi asilimia 28.2 mwaka 2012. Katika kutatua tatizo la umasikini, Serikali itaelekeza nguvu zaidi katika sekta ya viwanda na uboreshaji wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

1.2.4 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 4.0 Januari 2015 hadi asilimia 6.4 Julai 2015 na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 6.8 Desemba 2015. Mwenendo huu ulichangiwa kwa kiwango kikubwa na kuongezeka kwa bei za vyakula na kushuka kwa bei za nishati. Aidha, katika nchi za Afrika Mashariki mfumuko wa bei uliendelea kuwa katika kiwango cha tarakimu moja katika kipindi cha Januari 2015 hadi Desemba 2015. Matarajio ya Tanzania ni kubakiza mfumuko wa bei katika kiwango cha tarakimu moja kwa kuongeza uzalishaji hususan wa chakula na kuimarisha sera za kifedha na bajeti. **Kielelezo Na. 1.1** kinaonesha mwenendo wa mfumuko wa bei kwa kipindi cha Januari 2014 hadi Desemba 2015 ambapo kiwango cha chini kilikuwa asilimia 4.0 Januari 2015.

Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Januari 2014 – Desemba 2015)



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2016

1.2.5 Ujazi wa Fedha na Karadha

Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikuwa asilimia 16.6 kwa kipindi cha mwaka kilichoishia Oktoba 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 16.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Hii ilitokana na kuongezeka kwa rasilimali za benki, mikopo ya benki kwa sekta binafsi na Serikali kuendelea kukopa katika mabenki ya ndani. Katika kipindi kilichoishia Oktoba 2015, ukuaji wa kiwango cha mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi ilikuwa ni asilimia 24.6 ikilinganishwa na asilimia 22.3 Oktoba 2014. Mikopo iliyotolewa na benki za kibiashara katika kipindi kinachoishia Oktoba 2015 ni kama ifuatavyo: shughuli za biashara asilimia 21.1; watu binafsi asilimia 16.9; uzalishaji viwandani asilimia 11.4; kilimo asilimia 8.1; shughuli za mawasiliano na uchukuzi asilimia 7.9; majengo na ujenzi asilimia 4.8; na hoteli na migahawa asilimia 3.6.

1.2.6 Mwenendo wa Viwango vya Riba

Kiwango cha riba za amana za muda maalum kiliongezeka kutoka wastani wa asilimia 8.02 Oktoba 2014 hadi asilimia 9.41 Oktoba 2015. Aidha, kiwango cha riba za amana kiliongezeka hadi asilimia 10.92 Oktoba 2015. Vilevile, wastani wa kiwango cha riba za mikopo kiliongezeka kutoka asilimia 15.68 Januari 2015 hadi asilimia 16.11 Oktoba 2015. Kwa upande wa riba za amana za akiba, wastani uliongezeka kutoka asilimia 3.16 Januari 2015 hadi asilimia 3.45 Oktoba 2015. Tofauti kati ya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 3.43 Januari

2015 na kufikia asilimia 3.22 Oktoba 2015. Mwenendo huu wa viwango vya riba unaonesha kuendelea kuimarika kwa mazingira ya kupata mikopo na uwekezaji nchini. Aidha, juhudi zaidi zinahitajika ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara na ushindani nchini.

1.2.7 Thamani ya Shilingi

Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani iliendelea kupungua katika kipindi chote kuanzia Januari 2015 hadi Oktoba 2015, ambapo dola moja ya Kimarekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi 1,745.6 Januari 2015 na shilingi 2,177.1 Oktoba 2015. Kupungua kwa thamani ya shilingi kulitokana na kupungua mapato ya mauzo nje ya nchi hususan yatokanayo na dhahabu na utalii, kuongezeka kwa mahitaji makubwa ya dola ya kimarekani kwa ajili ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka nje na kuimarika kwa dola ya kimarekani dhidi ya sarafu nyingine za kimataifa.

Kielelezo Na. 1.2: Mwenendo wa Thamani ya Shilingi Januari 2015 hadi Oktoba 2015



Chanzo: Benki ya Tanzania, 2015

1.2.8 Urari wa Biashara

Katika mwaka unaoishia Oktoba 2015, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma nje ulikuwa wa kuridhisha ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2014. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 9.2 kutoka Dola za Kimarekani milioni 8,610.0 Oktoba 2014 hadi Dola milioni 9,406.1 Oktoba 2015. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii na mauzo ya bidhaa zisizo za asilia ambazo ni bidhaa za viwandani. Thamani ya mauzo ya bidhaa viwandani iliongezeka

kwa asilimia 8 kutoka dola za kimarekani milioni 1,215.8 Oktoba 2014 hadi dola za kimarekani milioni 1,313.5 Oktoba 2015. Thamani ya mapato yatokanayo na shughuli za usafiri na usafirishaji yaliongezeka kutoka dola za kimarekani milioni 1,988.6 Oktoba 2014 hadi dola za kimarekani milioni 2,237.5 Oktoba 2015. Aidha, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ilifikia dola za Kimarekani milioni 13,200.6 ikilinganishwa na dola za kimarekani milioni 13,487.5 Oktoba 2014. Hali hii ilitokana na kushuka kwa uagizaji wa nishati ya mafuta na bidhaa za viwandani. Uagizaji wa nishati ya mafuta ulishuka kutokana na kushuka kwa bei na kiwango cha mafuta yaliyoagizwa katika soko la Dunia. Hivyo, katika kipindi cha Oktoba 2014 hadi Oktoba 2015, urari wa biashara uliimarika kutoka nakisi ya Dola za Kimarekeni 4,972.3 hadi nakisi ya Dola za Kimarekani 4,002.0 katika kipindi husika.

1.2.9 Akiba ya Fedha za Kigeni

Katika kipindi kinachoishia Oktoba 2015, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka na kufikia dola za Kimarekani milioni 4,034.2. Kiasi hiki kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.0 bila kujumuisha uagizaji wa bidhaa na huduma kwa ajili ya uwekezaji wa moja kwa moja nchini. Kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni kumetokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi.

1.2.10 Mapato na Matumizi ya Serikali

Katika kipindi cha Julai 2014 hadi Juni 2015, jumla ya mapato ya Serikali yakijumuisha ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 11,013.0 sawa na asilimia 89 ya lengo la kukusanya bilioni 12,636.5. Mapato yatokanayo na kodi yalifikia shilingi bilioni 9,938.4 sawa na asilimia 87.8 ya lengo. Mapato ya kodi yamekuwa yakiongezeka kwa wastani wa asilimia 20 kila mwaka lakini kwa mwaka 2014/15 mapato ya kodi yaliongezeka kwa asilimia 6 tu. Malengo ya kodi hayakufikiwa kutokana na kushuka kwa shughuli za utafiti na utafutaji wa madini, mafuta na gesi ambazo hutozwa kodi ya zuio; kushuka kwa bei ya dhahabu na mafuta ya petroli katika soko la Dunia; mwitikio mdogo wa wananchi kutumia mashine za kieletroniki za ukusanyaji wa kodi na kushindwa kutekelezwa kwa maboresho yaliyopendekezwa katika kuongeza wigo wa mapato hususan katika tozo ya kadi za simu.

Kwa upande wa matumizi, katika kipindi cha Julai 2014 hadi Juni 2015, jumla ya matumizi yote yalikuwa shilingi bilioni 17,189.7 sawa na asilimia 87 ya

makadirio ya bajeti. Kati ya hizo, shilingi bilioni 13,928.0 zilitumika katika matumizi ya kawaida. Matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 3,261.7 chini kwa asilimia 51 ya makadirio ya bajeti ya maendeleo shilingi bilioni 6,473.0. Matumizi katika bajeti ya maendeleo hayakufikiwa kutokana na kutokufikiwa kwa malengo ya kukopa mikopo yenye masharti nafuu na washirika wa maendeleo kutotimiza ahadi zao kwa wakati. Aidha, katika mwaka 2015/16, fedha za maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni 5,906.95 na fedha zilizotolewa hadi Desemba 2015 ni shilingi bilioni 1,845.56. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 1,619.54 sawa na asilimia 38.2 ya bajeti ya fedha za maendeleo za ndani na fedha za nje ni shilingi bilioni 226.02 sawa na asilimia 13.6 ya bajeti ya fedha za maendeleo za nje.

1.2.11 Deni la Taifa

Hadi Oktoba 2015, deni la Taifa lilifikia dola za kimarekani milioni 19,221.4 ikilinganishwa na dola za kimarekani milioni 18,643.8 katika kipindi kinachoishia Oktoba 2014. Ongezeko hilo lilitokana na mikopo mipya yenye masharti nafuu na ya kibiashara na malimbikizo ya riba ya deni hususan kutoka nchi ambazo hazijatoa misamaha kwa mujibu wa makubaliano ya klabu ya Paris. Katika deni la Taifa, dola za kimarekani milioni 15,371.8 ni deni la nje sawa na asilimia 80 ya deni ambapo deni la ndani lilikuwa dola za kimarekani milioni 3,849.6 sawa na asilimia 20 ya deni. Mikopo hiyo ilielekezwa katika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo hususan miundombinu ya barabara na umeme.

SURA YA PILI

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

2.1 Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/15

2.1.1 Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa

(a) **Sekta ya Kilimo:** Lengo kuu lilikuwa ni kuongeza uzalishaji ambapo shughuli zilizotekelezwa ni: Kupata hatimiliki kwa mashamba makubwa manne yenye jumla ya hekta 117,800 ya Kitengule, Bagamoyo, Lukulilo na Mkulazi dhidi ya lengo la kupata mashamba manane ya uwekezaji katika mabonde ya Wami, Ruvu, Rufiji, Kagera, Kilombero na Malagarasi; na kupatikana kwa watoa huduma binafsi kwa ajili ya skimu 30 za umwagiliaji katika Wilaya za Mbarali, Kyela na Iringa ambapo uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka tani 4.1 hadi 5.0 kwa hekta.

(b) **Sekta ya Elimu**: Lengo kuu ni kuimarisha ubora wa elimu ambapo hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kukamilika ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule 167 sawa na asilimia 63.25 ikijumuisha maabara; ujenzi wa shule 97 sawa na asilimia 36.74; kutoa mafunzo kwa walimu 1,559 kutumia teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika masomo ya Sayansi na Hisabati; kutoa mafunzo kwa walimu 4,064 wa Hisabati, Baiolojia, Kiingereza na Kiswahili; kupatiwa mafunzo ya usimamizi wa shule kwa walimu 3,001; na kuongezeka kwa ufaulu wa shule za msingi na sekondari kutoka asilimia 31 na 43 mwaka 2012 hadi asilimia 57 na 70 mwaka 2014 kwa mtiririko huo.

(c) **Sekta ya Nishati:** Lengo kuu ni kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini ambapo kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa ujenzi wa bomba la gesi (km 542) kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam na ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi Madimba (Mtwara) na Songosongo (Lindi); kuunganisha umeme kwa wateja wapya 8,078 kupitia mradi wa usambazaji wa umeme vijijini awamu ya pili. Hadi Juni 2015, wateja waliounganishiwa umeme chini ya miradi ya REA na TANESCO imefikia 241,401; na kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za umeme kutoka asilimia 18 mwaka 2012 hadi asilimia 40 mwaka 2015.

(d) **Sekta ya Uchukuzi:** Lengo kuu ni kuimarisha usafiri na usafirishaji. Katika eneo la **Bandari,** hatua zilizofikiwa ni: kupungua kwa muda wa meli kukaa bandarini kwa ajili ya kupakia na kupakua mizigo kutoka siku 4.8 hadi 2.8 ikilinganishwa na lengo la siku 4; kuongezeka kwa

uwezo wa bandari kupakua magari kwa kila shifti moja ya saa 8 kutoka magari 800 hadi magari 859; kuongezeka kwa idadi ya shehena zilizohudumiwa na bandari ya Dar es Salaam kutoka tani milioni 10.3 hadi 14.6 ikilinganishwa na lengo la tani milioni 9.87. Katika eneo la **Reli,** mafanikio ni pamoja na: kukamilika kwa utandikaji wa reli nzito ya ratili 80/yadi kati ya stesheni za Kitaraka na Malongwe (km 89); kukamilika kwa ujenzi wa madaraja 3 kati ya stesheni za Bahi na Kintiku (km 517 kutoka Dar es Salaam) na madaraja 2 kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe (km 293 na km 303 kutoka Dar es Salaam); ukarabati wa eneo la reli kati ya Kilosa na Gulwe lililoathiriwa na mafuriko; ununuzi wa vichwa vipya vya treni 13, mabehewa mapya 22 ya abiria kwa ajili ya huduma ya treni maalum (Deluxe), mabehewa mapya ya mizigo 274, mabehewa ya breki 34 na mabehewa ya kokoto 25; kukamilika uundaji upya wa vichwa 10 vya treni, mabehewa ya mizigo 89 na mabehewa 31 ya abiria katika karakana ya Morogoro. Kwa ujumla uchukuzi wa mizigo kwa njia ya reli umeongezeka kwa asilimia 42 kwa mwezi.

(e) **Sekta ya Maji:** Lengo kuu ni kuwezesha upatikanaji wa maji safi na salama hususan maeneo ya vijijini**.** Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kukamilika ujenzi wa miradi ya maji 975. Idadi hii imenufaisha wananchi milioni 5.75 ambapo jumla ya vituo 24,129 vya kuchotea maji vimejengwa katika Halmashauri 148; na kuanzisha Jumuiya za Watumia Maji (COWSOs) 1,802 ambapo Jumuiya 875 zimesajiliwa na kutoa huduma za maji vijijini kwa ufanisi.

(f) **Utafutaji wa Rasilimali Fedha:** Lengo kuu ni kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha ambapo utekelezaji ni pamoja na: kuanza kutumia kanzidata bora inayohifadhi taarifa na kuthaminisha bidhaa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, hivyo kutoa makadirio bora zaidi ya viwango vya kodi; na kuanza kutoza Tozo maalumu kwa ajili ya uwekezaji katika elimu ikiwa ni asilimia 2.5 ya mapato ghafi ya kampuni za simu.

2.1.2 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati

2.1.2.1 Miundombinu

A. Reli

(a) **Mradi wa kubadilisha km 197 za njia ya reli kwa kuweka reli ya kiwango cha ratili 80 kwa yadi:** Kuendelea na ukarabati wa mgodi wa kokoto wa Tura - Tabora na mitambo yake ambayo itawezesha

uzalishaji wa kokoto kwa ajili ya matengenezo ya njia za reli na kuendelea na taratibu za zabuni ya kutandika reli kati ya Igalula na Tabora (km 37) na kati ya Dar es Salaam na Munisagara (km 52).

(b) **Mradi wa uboreshaji wa njia ya Reli ya TAZARA:** Kukarabati mtambo wa kuzalisha kokoto wa Kongolo – Mbeya na kubadilishwa mataruma 8,900 ya zege na 3,422 ya mbao.

(c) **Mradi wa usafiri wa Treni ya Abiria Dar es Salaam:** Kusainiwa mkataba na kampuni ya GIBB ya Afrika ya Kusini kwa ajili upembuzi yakinifu wa njia mpya za reli jijini Dar es Salaam kwenda maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Bagamoyo.

B. Bandari

(a) **Bandari ya Dar es Salaam:** Kukamilisha taarifa ya uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya kuimarisha gati Na. 1–7 ikijumuisha ujenzi wa gati Na. 4 la magari; kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa kubadili gati Na. 5-7 kuwa gati la makasha (*container terminal*). Mshauri Mwelekezi pia atafanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati Na. 13 na 14.

(b) **Bandari ya Mtwara:** Kuanza maandalizi ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa magati manne kwa awamu. Awamu ya kwanza itaanza kwa kujenga gati moja lenye urefu wa mita 300 kwa kutumia fedha za ndani. Aidha, kampuni binafsi ya Dangote itajenga gati la tano katika eneo la Kisiwa mkoani Mtwara ambapo kwa sasa majadiliano kati ya Mamlaka ya Bandari na kampuni hiyo yameanza.

(c) **Bandari ya Mbegani – Bagamoyo:** Kusainiwa kwa makubaliano ya awali (MoU) Oktoba 2014 kati ya wabia watatu ambao ni Serikali, Kampuni ya China *Merchants Holding International na General State Reserve Funds* ya Oman kwa ajili ya ujenzi wa bandari.

(d) **Bandari ya Mwambani, Tanga:** Kupitia upya taarifa ya upembuzi yakinifu kwa lengo la kuiboresha kwa kujumuisha matarajio ya kuongeza shehena ili kuvutia wawekezaji. Mradi huu utatangazwa upya kwa wazabuni baada ya maboresho ili kupata wawekezaji binafsi.

(e) **Bandari za Maziwa Makuu**

(i) **Bandari za Ziwa Tanganyika:** Kuanza ujenzi wa gati katika bandari ndogo za Kagunga na Kibweza; kumtafuta Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuendeleza bandari ndogo ya Kerema; kuendelea na majadiliano na Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa gati la bandari ndogo ya Lagosa; na kukamilika kwa tathmini ya mazingira kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria katika

bandari kubwa ya Kigoma.

(ii) **Bandari za Ziwa Victoria:** Kuendelea na ujenzi wa magati ya bandari ndogo za Lushamba na Kome ambapo ujenzi umefikia asilimia 50 na kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa bandari kubwa tano za Mwanza, Bukoba, Kemondo Bay, Musoma na Nansio pamoja na bandari ndogo 15.

(iii) **Bandari za Ziwa Nyasa:** Kuendelea na ujenzi wa gati la bandari kubwa ya Itungi ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 90; na kuanza kazi ya kuhamisha chelezo kutoka Mwanza na kuifunga katika bandari ya Itungi.

C. Barabara

(a) Mradi wa Barabara Kuu: Kukamilika kwa ujenzi wa kilometa 542.6 za barabara kuu kwa kiwango cha lami ikilinganishwa na lengo la kilometa 560.3 na ukarabati wa kilometa 102.09 za barabara kuu kwa kiwango cha lami ikilinganishwa na lengo la kilometa 131.5.

(b) Mradi wa Barabara zenye kufungua Fursa za Kiuchumi:

(i) **Barabara zilizokamilika**: Tunduma – Sumbawanga (km 223.2); Ndundu - Somanga (km 60); Lwanjilo – Chunya (km 36) na Iringa – Dodoma (km 259.8);

(ii) **Barabara zinazoendelea kujengwa**:

- Itoni – Mkiu – Ludewa – Manda (km 211) ujenzi umeanza; Sumbawanga –Mpanda - Nyakanazi (km 770.9) na Kidahwe - Nyakanazi (km 310): sehemu ya Sumbawanga - Kanazi (km 75) ujenzi umefikia asilimia 68.6; Kanazi – Kizi - Kibaoni (km 76.6) asilimia 43.55; Sitalike – Mpanda (km 39.9) asilimia 76; Kidahwe – Kasulu ujenzi (km 50) ujezi umefikia asilimia 10; na Kibondo - Nyakanazi (km 50) asilimia 11.95.
- Mbeya – Makongorosi - Mkiwa (km 528): sehemu ya Mbeya – Lwanjilo (km 36) ujenzi umefikia asilimia 86; Manyoni – Itigi – Tabora (km 264.35): sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35) ujenzi umefikia asilimia 98.25; Nyahua – Tabora (km 85) asilimia 86.7;
- Dodoma – Babati (km 251.4); sehemu ya Dodoma – Mayamaya km (43.65) ujenzi umefikia asilimia 80; Mayamaya – Mela (km 99.35) asilima 24; na Mela – Bonga (km 88.8) asilimia 24.2;

- Masasi - Songea – Mbamba Bay (km 1,154.7); sehemu ya Mangaka – Nakapanya – Tunduru (km 137) ujenzi umefikia asilimia14.8; Mangaka – Mtambaswala km (65.5) asilimia 18.4; Namtumbo – Kilimasera (km 60.7) asilimia 30.8; Kilimasera – Matemanga (km 68.2) na Matemanga – Tunduru (km 58.7) ujenzi umeanza; Mwigumbwi – Maswa – Bariadi - Lamadi (km 171.8): ujenzi umefikia asilimia 93 na

(iii) **Barabara zilizo katika hatua ya upembuzi yakinifu/usanifu wa kina**: Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396); na Bagamoyo (Makurunge) - Sadani – Tanga (km 178).

(c) Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani:

(i) **Barabara zilizokamilika** ni Arusha – Namanga (km 105), Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5) na Isaka – Ushirombo (km 132).

(ii) **Barabara zinazoendelea ni pamoja** na: Nyanguge – Musoma (km 183) na mchepuko wa Usagara – Kisesa (km 17) na Bulamba – Kisorya (km 51); Isaka – Lusahunga (km 242) na Nyakasanza – Kobero (km 60): sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110) ujenzi umefikia asilimia 51, Lusahunga – Rusumo (km 92) na Nyakasanza – Kobero usanifu wa kina umekamilika; Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112): ujenzi umefikia asilimia 52.2, Arusha – Moshi – Holili na Arusha Bypass (km 140) mkandarasi wa ujenzi amepatikana.

(d) Barabara za Mikoa: Kukamilika kwa ujenzi wa km 51.7 kwa kiwango cha lami sawa na asilimia 52.3 ya lengo la mwaka na kukarabati km 343.8 kwa kiwango cha changarawe sawa na asilimia 21.5 ya lengo.

(e) Barabara za Kupunguza Msongamano Mijini (km 109.35):

(i) **Barabara zilizokamilika:** Ubungo Bus Terminal – Mabibo - Kigogo Roundabout (km 6.4); Jet Corner – Vituka – Devis Corner (km 10.3); Ubungo Maziwa – External (km 2.25); Kibamba – Mloganzila (km 4).

(ii) **Barabara zinazoendelea kujengwa:** Kigogo Roundabout - Bonde la Msimbazi - Twiga/Msimbazi Junction (km 2.7) ujenzi umefikia asilimia 86; Tabata Dampo – Kigogo (km 1.65) asilimia 72 na Mbezi (Morogoro Road) – Malambamawili - Kinyerezi - Banana (km 14) asilimia 67; Tegeta Kibaoni -

Wazo – Goba - Mbezi Mwisho (km 20) asilimia 56; Tangi Bovu - Goba (km 9) asilimia 54; Kimara Baruti – Msewe - Changanyikeni (km 2.6) asilimia 39; na ujenzi wa mradi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka na vituo vyake upo katika hatua za mwisho za utekelezaji.

(f) **Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyover):** Kusainiwa kwa mkataba na mkandarasi wa ujenzi wa barabara za juu eneo la TAZARA; kukamilika kwa tathmini ya mali katika eneo la mradi wa barabara ya juu katika makutano ya Ubungo; na kuendelea na usanifu wa kina kwa barabara ya Nyerere kuanzia eneo la TAZARA hadi Uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere - JNIA.

(g) **Mradi wa Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (km 200):** Kupatikana kwa Mtaalam Mshauri ambaye anaendelea na kazi ya usanifu wa kina ili kuwezesha kuanza utekelezaji wa mradi.

(h) **Madaraja:** Kuendelea na ujenzi wa madaraja 6 ambapo daraja la Mbutu limefikia asilimia 99, Kigamboni asilimia 92, Kavuu asilimia 40, Kilombero asilimia 27.58, Lukuledi II asilimia 90 na Sibiti asilimia 22; kukamilika taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kupitia usanifu wa nyaya zinazoshikilia daraja *(design review of cable strays)* na kusimamia kazi ya ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara); kuendelea na usanifu wa daraja la Ruhuhu (Ruvuma); na kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa madaraja ya Selander na Momba.

(i) **Vivuko na Maegesho:** Ununuzi wa kivuko kipya kitakachotumika kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo; ujenzi wa maegesho ya Iramba na Majita mkoani Mara na vituo vitatu vya Luchelele, Igogo na Sweya kwa ajili ya kivuko kiendacho kasi ili kupunguza msongamano jijini Mwanza; na kuendelea na ujenzi wa maegesho ya kivuko katika eneo la Magogoni (Dar es Salaam) na Mbegani (Bagamoyo).

D. Nishati

(a) **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam (km 542):** Kukamilika kwa ujenzi wa bomba la gesi na mitambo ya kusafisha gesi katika maeneo ya Madimba na Songosongo; na kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 32 zenye uwezo wa kuhudumia wafanyakazi 172 katika maeneo ya Madimba na Songosongo;

(b) **Mtambo wa Kufua Umeme Kinyerezi I (MW 150):** Kukamilika kwa usimikaji wa mitambo 4 ya kufua umeme yenye uwezo wa kuzalisha MW 150 na kuanza majaribio ambapo mtambo mmoja unafanya kazi

na kuzalisha MW 40 zinazoingizwa kwenye gridi ya Taifa; kukamilika kwa ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kV 220 kutoka Kinyerezi hadi Kimara na njia ya umeme wa msongo wa kV 132 kutoka Kinyerezi hadi Gongo la Mboto;

(c) **Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo kV 220 Makambako – Songea (km 250):** Kulipa fidia ya shilingi bilioni 6.72 kwa wananchi 1,804 katika Mikoa ya Njombe na Ruvuma. Kiasi cha fidia kilichobaki ni shilingi milioni 4.41 kwa wananchi 8 wa mikoa hiyo.Vile vile, kazi ya usanifu wa njia ya kusambaza umeme inaendelea;

(d) **Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 Iringa - Shinyanga (km 670)**: Ujenzi wa nguzo 480 kati ya 594 kwa Lot Na. 1, nguzo 78 kati ya 586 kwa Lot Na. 2 na nguzo 361 kati ya 594 kwa Lot Na. 3. Hatua itakayofuata ni utandikaji wa nyaya ili kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa;

(e) **Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 *North West Grid* (Mbeya – Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi km 1,148):** Kuboresha upembuzi yakinifu na usanifu wa kubadilisha msongo wa umeme kutoka kV 220 hadi kV 400 unaotekelezwa na kampuni ya SWECO ya Sweden; na kukamilika kwa upimaji wa kilomita 321 za mkuza wa njia ya umeme kutoka Mbeya hadi Sumbawanga;

(f) **Mradi wa msongo wa kV 400 North - East Grid (Dar es Salaam – Tanga – Arusha km 682):** Kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi wa mradi; na kuendelea na upimaji ardhi na kuweka mipaka ya eneo la mradi kutoka Kinyerezi (Dar es Salaam) hadi Chalinze (Pwani). Vile vile, fidia kiasi cha shilingi milioni 470 imelipwa kwa wananchi 37 katika kituo cha Kibaha ikilinganishwa na tathmini ya awali ya shilingi bilioni 21.4 kwa maeneo ya mkoa wa Pwani;

(g) **Mradi wa kusambaza umeme katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Shinyanga na Geita *(Mradi wa Electricity V):*** ukarabati wa vituo katika maeneo ya Ilala umefikia asilimia 98; ufungaji wa mitambo katika kituo cha Ilala umefikia asilimia 14; ujenzi wa msingi katika kituo cha sokoine umekamilika kwa asilimia 70; na kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa kituo cha Njiro ambapo ufungaji wa mitambo umefikia asilimia 25;

(h) **Miradi ya Umeme Vijijini *(REA Turnkey Phase II):*** Kuunganishwa kwa wateja wapya 30,173 katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita, Katavi, Kilimanjaro, Mara, Njombe, Lindi, Mtwara, Iringa, Singida, Tanga, Kagera, Kigoma, Morogoro, Rukwa, Shinyanga, Mbeya,

Tabora na Simiyu.

E. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

(a) **Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano:** Ujenzi na upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano awamu ya I na II ambapo hadi sasa km 7,560 zimekamilika katika mikoa 24 ya Tanzania Bara; kukamilika kwa ujenzi wa Mikongo ya mijini katika mikoa ya Mwanza (km 36) na Arusha (km 58) na kuendelea na ujenzi katika mikoa ya Morogoro (km 18), Dodoma (km 42), Kilimanjaro (km 35.08) na Tanga (km 43.28); na kuendelea na ujenzi wa jengo la Data Center katika eneo la Kijitonyama; kuendelea na kazi ya kuunganisha Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; kuiunganisha Tanzania na mikongo ya baharini ya SEACON na EASSy na kutoa maunganisho ya mawasiliano kwa nchi za jirani zikiwemo Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi; na kutoa huduma za maunganisho kwenye mkongo wa kimataifa wa SEAS (Seychelles East Africa System) unaounganisha nchi za Seychelles na Tanzania na Dunia kwenye mikongo mingine ya Kimataifa.

(b) **Maeneo Maalum ya TEHAMA (*ICT Park*):** Kukamilika kwa malipo ya fidia ya shilingi bilioni 1.7 kwa wananchi 9 na taasisi 2 katika eneo lenye ukubwa wa ekari 438 lililopo EPZ Bagamoyo.

F. Maji

(a) **Mradi wa Maji wa Ruvu Chini – Pwani**: Ulazaji wa mabomba kutoka eneo la mradi (Bagamoyo) hadi Dar es Salaam umekamilika kwa asilimia 97; na kukamilika kwa ukarabati wa matanki ya kuhifadhia maji yaliyopo Chuo Kikuu Ardhi. Aidha, mradi huu utaongeza uwezo wa uzalishaji maji katika jiji la Dar es Salaam kutoka lita milioni 180 hadi lita milioni 270 kwa siku ambapo mahitaji ya jiji la Dar es Salaam kwa siku ni lita milioni 450.

(b) **Mradi wa Maji Ruvu Juu – Pwani**: Upanuzi wa chanzo cha maji eneo la Ruvu Darajani na mitambo ya kusafisha maji eneo la Mlandizi unaendelea ambapo ujenzi umefikia asilimia 70. Vile vile, ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara na ujenzi wa tanki la Kibamba umefikia asilimia 45.

(c) **Mradi wa Visima Virefu vya Kimbiji - Dar es Salaam na Mpera - Pwani:** Kukamilika kwa uchimbaji wa visima 6 kati ya 20 ambapo visima 3 vimechimbwa Kimbiji na visima 3 Mpera. Aidha, mkandarasi amechimba visima 8 vya uchunguzi wa mwendo wa maji chini ya

ardhi katika maeneo ya Chanika, Mkuranga, Amani Gomvu, Mwasonga, Kimbiji, Kibada, Buyuni na Amadori.

(d) **Miradi ya Maji Vijijini**: Kukamilika kwa miradi mipya 975 ya maji ya vijiji 10 katika vijiji 1,206 yenye vituo 24,129 vya kuchotea maji katika Halmashauri 148. Miradi hiyo imewanufaisha wananchi milioni 5.75 na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na kufikia wananchi 21,783,062 sawa na asilimia 68.8.

(e) **Upanuzi wa Mradi wa Maji Ziwa Victoria – Shinyanga – Kahama**: Kukamilika kwa usanifu wa ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya miradi ya maji kwa miji ya Tabora, Igunga na Nzega.

(f) **Miradi ya Maji ya Kitaifa**: Serikali imeendelea kuhudumia miradi ya Maji ya Kitaifa katika maeneo ya Makonde, Wanging'ombe na *Handeni Trunk Main* kwa kukarabati miundombinu ya maji, ununuzi wa pampu, mabomba na kugharamia umeme kwa ajili ya kuendesha mitambo.

2.1.2.2 Kilimo

A. Kilimo cha Mazao

(a) **Uwekezaji katika Kilimo cha Miwa na Mpunga**: Kuhakikiwa kwa mipaka ya mashamba matatu ya Muhoro, Mahurunga na Tawi na kuanza kwa taratibu za uhaulishaji (recategorisation) wa mashamba hayo; kupatikana kwa hatimiliki ya shamba la Kasulu ambapo itatolewa baada ya kukamilika kwa zoezi la upimaji; kuhakikiwa kwa jumla ya hekta 43,200 za mashamba ya wakulima wadogo na kuandaa hatimiliki za Kimila 1,513 kwa wakulima wanaozunguka mashamba ya Lukulilo na Ngalimila; na kukamilika kwa mpango-kina wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji vinavyozunguka mashamba ya Bagamoyo na Mkulazi.

(b) **Skimu 78 za Umwagiliaji Mpunga:**

(i) Ujenzi wa skimu 19 zenye jumla ya hekta 9,709 ambapo wananchi 69,681 wamenufaika dhidi ya lengo la kuendeleza skimu 39 zenye jumla ya hekta 21,738;

(ii) Usanifu wa maghala manane katika skimu nane za umwagiliaji na kupatikana kwa wakandarasi wa ujenzi;

(iii) Kupatikana kwa watoa huduma binafsi kwa ajili ya skimu 30 za umwagiliaji; na

(iv) Kupata Hatimiliki za Kimila 723 kwa wakulima wadogo katika skimu za umwagiliaji za Msolwa Ujamaa na Mvumi.

(c) **Kilimo cha Mahindi:** kukamilisha ujenzi wa maghala mapya mawili

katika Wilaya ya Mlele na Nsimbo ambapo lengo lilikuwa ni kujenga maghala 10; kukamilisha ukarabati wa maghala 36 dhidi ya lengo la maghala 55 katika Wilaya za Iringa, Njombe na Songea; na kupatikana kwa Mtaalam Mwelekezi wa kujenga mfumo wa kanzidata ya COWABAMA kwa ajili ya kurahisisha uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko kwa wadau.

(d) **Tafiti za Kilimo:-**

(i) Kuzalisha na kusambaza miche bora ya kahawa 1,014,671 katika wilaya za Moshi, Mbinga, Bukoba, Mbozi (Mbimba) na Tarime (Sirari);

(ii) Kuidhinisha aina mpya 48 za mbegu za mazao kutoka vituo vya utafiti vya umma ambapo 24 ni mbegu bora za korosho chotara na mahindi (4), ngano (3), mbaazi (4), Kunde (2), muhogo (4), ufuta (1), korosho (24), miwa (5) na pamba (1);

(iii) Kuidhinisha aina mpya 17 za mbegu za mtama (2), mahindi (12) na tumbaku (3) zilizozalishwa na sekta binafsi;

(iv) Kuendelea na maboresho ya kituo cha Kilimo cha Mpunga cha KATRIN kilichopo wilayani Kilombero (Morogoro) ambapo ukarabati wa miundombinu umefikia asilimia 74;

(v) Kukamilika kwa ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 35 za mashamba ya utafiti ya vituo vya KATRIN na Ukiriguru; na

(vi) Ukarabati wa miundombinu ya umeme katika kituo cha utafiti cha Dakawa umefikia asilimia 50.

(e) **Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhi Chakula:** Kukamilika kwa ujenzi wa ghala 1 kati ya maghala 2 katika halmashauri ya Songea na ujenzi wa ghala katika halmashauri ya Mbozi umefikia asilimia 40.

B. Mifugo

(a) **Miundombinu ya Maji na Malisho:** Kuanishwa kwa maeneo yatakayochimbwa malambo kwa ajili ya kunywesha mifugo katika wilaya 3 za Msomera (Handeni), Pangalua (Chemba) na Masisu (Ngorongoro); na kuainishwa na kutengwa maeneo ya ufugaji yatakayotumika kuanzisha shamba darasa la kufundishia wafugaji kuhusu uzalishaji, uvunaji na uhifadhi wa malisho katika Wilaya za Busega, Igunga na Kiteto.

(b) **Vituo vya Uhamilishaji**: Uagizwaji wa vifaa vya uhamilishaji ikiwemo mitungi 9 kwa ajili ya kituo cha Sao Hill na ukarabati wa mashine ya kukamulia maziwa pamoja na ununuzi wa mbegu za

malisho; ukarabati wa bwawa la mifugo la shamba la mitamba Nangaramo; ukarabati wa mashine ya kukamulia maziwa katika shamba la mitamba la Kitulo; kuagizwa mitamba 30 kutoka Kenya kwa ajili ya shamba la Ngerengere, mitamba 45 kwa shamba la Mabuki na mbegu bora za malisho; na kupatiwa hatimiliki kwa shamba la mitamba la Nangaramo lenye hekta 56,337.

(c) **Ujenzi wa Minada na Masoko:** Ukarabati wa minada ya Pugu (Ilala), Lumecha (Songea), Kirumi (Butiama) na Nyamatala (Misungwi); kukamilika kwa barabara ya kuzunguka mnada wa upili wa Kizota (Dodoma) na ukarabati wa nyumba za watumishi na kusimika mzani; kukamilika kwa ujenzi wa ofisi, mazizi na barabara ya kuingilia mnadani, sehemu ya kunadia mifugo katika mnada wa upili wa Kasesya (Kalambo); na kusimika mizani ya mifugo katika minada ya upili 11 na uhamasishaji juu ya matumizi yake.

(d) **Upatikanaji wa Pembejeo za Mifugo:** Ununuzi wa lita 119,349 za dawa za kuogesha mifugo kupitia mpango wa ruzuku ya asilimia 40 na kusambazwa katika mikoa 21; na ununuzi wa dozi 700,000 za chanjo ya kudhibiti ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo na kusambazwa kupitia vituo vya kanda katika Mikoa ya Arusha (350,000), Mara (100,000), Pwani (110,000) na Dodoma (140,000).

C. Uvuvi

(a) Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi: taratibu za kupata mtalaam mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kutambua eneo na aina ya bandari ya uvuvi zipo katika hatua za mwisho ambapo andiko la mradi litaandaliwa kwa ajili ya kuomba ufadhili wa ujenzi.

(b) Huduma ya Uzalishaji wa Samaki: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa vituo vya uvuvi vya Kisiju-Mkuranga, Chuno na Msimbati (Mtwara); kuimarishwa kwa kituo cha Machui (Tanga) kwa kujenga mabwawa 2 ya kufugia samaki, kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kutotolea vifaranga (*hatchery*) na mnara wa kuwekea matangi ya maji; na kuanzishwa kwa vituo 2 vya Mwamapuli – Igunga (Tabora) na Nyengedi (Lindi) na kuimarishwa kwa vituo vya Luhira (Ruvuma) na Kingolwira (Morogoro) vya ukuzaji viumbe kwenye maji baridi.

2.1.2.3 Viwanda

(a) Maeneo Maalum ya Uwekezaji

Bagamoyo SEZ: Ulipaji wa fidia ya shilingi bilioni 7 ambapo jumla

ya fidia iliyolipwa hadi sasa ni shilingi bilioni 26.64 kati ya shilingi bilioni 47.5; na kuingia mkataba wa utatu na kampuni za *China Merchant Holding International* (CMHI) ya Hongkong na State General Reserve Fund (SGRF) ya Oman wa kuwekeza katika eneo la Bagamoyo SEZ katika eneo la hekta 2,500, kati ya hizo, eneo la viwanda ni hekta 1,700 na bandari ni hekta 800.

(b) **Kituo cha Biashara na Uwekezaji Kurasini, Dar es Salaam:** Ulipaji wa fidia ya shilingi bilioni 53 na hivyo kukamilisha fidia iliyokadiriwa kulipwa mwaka 2013 ya shilingi bilioni 94.1. Hata hivyo, kiasi cha shilingi bilioni 3.79 kinahitajika kwa ajili ya fidia ya maeneo ambayo yalikuwa na mapungufu na kusafisha eneo kwa ajili ya uwekezaji.

(c) **Mradi wa Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga:** Kukamilika kwa ukarabati wa barabara ya Itoni - Mkiu – Liganga na Mchuchuma kwa kiwango cha changarawe; kukamilika kwa uthamini wa mali za wananchi shilingi bilioni 13.4 watakaopisha eneo la mradi Mchuchuma na Liganga na kuendelea na mazungumzo kati ya wawekezaji (Tanzania – China Mineral Resources Limited) na TANESCO juu ya mkataba wa kuuza umeme utakaozalishwa Mchuchuma.

(d) **Kiwanda cha Viuadudu Kibaha, Pwani:** Kukamilika ufungaji wa mitambo ya kiwanda na kuanza uzalishaji wa viuadudu kwa ajili ya kuua viluwiluwi vya mbu. Aidha, ujenzi wa barabara ya kuingilia kiwandani kwa kiwango cha lami imekamilika;

2.1.2.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu

A. Maendeleo ya Ujuzi Maalum

Kutoa mafunzo katika fani za mafuta na gesi kwa ngazi mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa wanafunzi 159. Kati ya hao wanafunzi 124 wanagharamiwa na Serikali na wanafunzi 35 wanagharamiwa na nchi wahisani.

B. Elimu na Mafunzo ya Ufundi

(a) **Vyuo Vikuu:** Shilingi 135,803,000,000 zimetolewa kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ikilinganishwa na lengo la shilingi 247,341,409,579 kwa robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2015/16 ambapo shilingi 134,685,646,257 zimetolewa kwa wanafunzi 119,073; kukamilisha jengo la umwagiliaji na kusimika mitambo katika maabara ya uhandisi wa umwagiliaji katika Chuo cha Ufundi Arusha; na kuendelea na ujenzi wa jengo la hospitali ya kufundishia ghorofa ya 9

katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Dar es Salaam - Kampasi ya Mlonganzila**.**

(b) **Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi:** Kukamilisha taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo 4 vya mafunzo ya ufundi katika mikoa ya Simiyu, Geita, Njombe na Rukwa.

(c) **Elimu ya Msingi na Sekondari:** Kutoa mafunzo kwa walimu 630 katika Halmashauri 40 nchini; kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya madarasa, vyoo, maabara na nyumba za walimu katika shule za msingi 528; kupatiwa mafunzo kwa walimu 5,868 wa masomo ya Sayansi, Hisabati, Biolojia na Lugha.

C. Afya na Ustawi wa Jamii

(a) **Hospitali ya Taifa Muhimbili**: kuendelea na ujenzi wa jengo la dharura kwa watoto na ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya Kituo cha Tiba na Mafunzo ya Upasuaji wa Moyo na kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kibingwa;

(b) **Taasisi ya Mifupa Muhimbili:** Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la ghorofa 7 litakalokuwa na sehemu za kutolea huduma pamoja na malazi kwa wagonjwa.

(c) **Taasisi ya Saratani Ocean Road**: kutoa vifaa tiba kwa ajili ya hospitali na kuanza ujenzi wa vyumba maalum (bunkers) kwa ajili ya kusimika mashine za kisasa kwa ajili ya kutolea tiba ya mionzi;

(d) **Hospitali za Rufaa za Kikanda**: Kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa kanda ya kati iliyopo Singida; kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la tiba ya mionzi katika Hospitali ya Bugando na ununuzi wa vifaa tiba; ukarabati wa wodi 6 katika hospitali ya Kibong'oto; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la X-rays katika hospitali ya Rufaa ya Mbeya; kuanza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje la hospitali ya Kanda ya Kusini-Mtwara; na

(e) Hospitali ya Kisasa ya Benjamin Mkapa Ultra Modern Hospital Dodoma: Kukamilika kwa ujenzi wa hospitali kwa ajili ya kutoa huduma za kibingwa za uchunguzi na tiba ya magonjwa. Hospitali itatumika kwa tafiti na mafunzo kwa wanafunzi wa afya wanaosoma katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

2.1.2.5 Huduma za Utalii, Biashara na Fedha

A. Utalii

Kuendelea na usanifu wa ujenzi wa Utalii House awamu ya pili eneo la ubalozi wa zamani wa Marekani na kuboreshwa kwa mfumo wa ukusanyaji mapato ya utalii, uwindaji na upigaji picha. Aidha, idadi ya watalii kutoka nje imeongezeka kutoka watalii 1,095,884 mwaka 2013 hadi watalii 1,140,156 mwaka 2014; na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii kutoka dola za Kimarekani bilioni 1.86 mwaka 2013 hadi dola za Kimarekani bilioni 2.01 mwaka 2014.

B. Biashara na Masoko

Kupitishwa kwa sheria ya mfumo wa stakabadhi za ghala; kuanzishwa kwa kampuni ya *Tanzania Mechantile Exchange Public Limited Company* kwa ajili ya kusimamia na kuendesha soko la mazao ya bidhaa; kuendeleza miundombinu ya masoko ya mikoa na kuanzisha masoko katika vituo vya mipakani ili kukuza biashara ya ndani na kikanda; kupanua matumizi ya simu viganjani katika kutoa taarifa za bei ya mazao na masoko kwa wakati; na kuendeleza na kukuza mauzo nje kupitia vituo vya kibiashara vya Dubai na London.

C. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

Vituo vya utoaji huduma za pamoja mipakani: Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya utoaji huduma za pamoja mipakani vya Sirari/Isebania, Holili/Taveta na Namanga (Tanzania/Kenya), Mtukula/Mutukula (Tanzania na Uganda), Rusumo (Tanzania na Rwanda) na Horohoro/Lungalunga (Tanzania na Kenya). Kuendelea na ujenzi wa kituo cha Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi). Vilevile, ujenzi wa kituo cha Songwe/Kasumulu upo katika hatua za mwisho za kumpata mkandarasi kwa ajili ya usanifu. **Majengo ya Ubalozi:** ununuzi wa majengo mawili jijini Paris, Ufaransa kwa ajili ya Ofisi na Makazi ya Balozi wa Tanzania pamoja na ukarabati wa jengo la Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Jijini New York; na kuendelea na ukarabati wa jengo la Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Maputo.

D. Huduma za Fedha

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania: Kuidhinishwa kwa Kanuni za Utumishi, Muundo wa Utumishi na Kanuni za Fedha za benki, kuendelea kwa taratibu za kukamilisha masharti ya upatikanaji wa leseni ya kudumu ya shughuli za kibenki. **Benki ya Rasilimali**

Tanzania: Serikali imeshaweka mtaji wa shilingi 152,137,661,000; benki imetoa mikopo ya shilingi 413,044,192,000; benki imefungua matawi Dar es Salaam (2), Arusha (1), Mwanza (1), Mbeya (1); na kupata leseni ya muda kutoka Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kuanzisha benki mpya ya biashara: **Benki ya Wanawake Tanzania:** Kuongeza mali za benki kutoka shilingi bilioni 26.5 hadi shilingi bilioni 34.8; kuanza kutoa huduma za kibenki katika mikoa ya Dodoma na Njombe (Makambako); na kutoa mikopo kwa wananchi hadi kufikia bilioni 19.2 ambapo idadi ya wanawake waliopewa mikopo walikuwa 25,557 sawa na asilimia 89 na wanaume 3,159 sawa na asilimia 11. **Vikundi vya Wajasiriamali Wadogo:** Kusajili vikundi vya SACCOS 5,559 na kufikisha idadi ya watu 1,153,248 ya waliojiunga na kunufaika na huduma za SACCOS; kuongezeka kwa mikopo inayotolewa na SACCOS kwa wanachama hadi kufikia shilingi bilioni 893; na kuanzishwa kwa VICOBA 23,000 vyenye wanachama 700,000 na kutoa mtaji wa shilingi bilioni 86 kwa VICOBA.

2.2 Ushiriki wa Sekta Binafsi

Mwaka 2014, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kilisajili miradi 704 yenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 11.9 ikilinganishwa na miradi 885 yenye thamani ya dola za Kimarekani 88.2 mwaka 2013. Kupungua kwa idadi ya miradi kulitokana na uwekezaji mdogo katika sekta ya kilimo na ufugaji, utalii, majengo na biashara. Aidha, fursa za ajira zilizopatikana kutokana na miradi iliyosajiliwa mwaka 2014 zilikuwa 68,442 ikilinganishwa na fursa za ajira 202,487 mwaka 2013. Kati ya miradi iliyosajiliwa mwaka 2014, miradi ya wageni ilikuwa 213, miradi ya wazalendo ilikuwa 323 na miradi ya ubia ilikuwa 168.

Mwaka 2014, sekta ya uzalishaji viwandani ndiyo iliyovutia zaidi wawekezaji, ambapo kulikuwa na miradi mipya 208 ikilinganisha na miradi mipya 225 mwaka 2013. Sekta zilizofuata kwa kusajili miradi mipya mingi mwaka 2014 ni: usafirishaji (142), majengo ya biashara (103); na shughuli za utafiti (100). Aidha, sekta ya mawasiliano ndiyo iliyokuwa na miradi yenye thamani kubwa zaidi mwaka 2014 kwa kiasi cha dola za Kimarekani milioni 7,141.2 ikifuatiwa na viwanda dola milioni 1,483.4, usafirishaji dola milioni 967.5 na majengo ya biashara dola 899.

2.3 Changamoto na Hatua za Kukabiliana

Katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kulijitokeza changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(a) Upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
(b) Taratibu ndefu na gharama kubwa za ununuzi wa umma;
(c) Madeni mengi, hususan ya wakandarasi wa ujenzi wa barabara;
(d) Urasimu wa upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji na hati miliki;
(e) Upatikanaji wa fedha za kulipa fidia na mapungufu katika taarifa za tathmini ya fidia na hivyo kucheleweshа ulipaji fidia kwa wakati;
(f) Bajeti ya maendeleo kutegemea kwa kiwango kikubwa misaada na mikopo kutoka nje;
(g) Kutojulikana kikamilifu kwa mchango wa sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
(h) Mazingira yasiyo wezeshi kwa uwekezaji na uendeshaji biashara; na
(i) Uhaba wa miundombinu wezeshi (barabara, maji na umeme) ya kuwezesha utekelezaji wa miradi.

Hatua za kukabiliana na changamoto hizo ni pamoja na:

(a) Kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha, hususan fedha za miradi ya Matokeo Makubwa Sasa na miradi ya Kitaifa ya Kimkakati;
(b) Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi au uwekezaji wa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma;
(c) Kupanua ushirikishwaji wa jamii katika hatua zote za maandalizi ya Mpango ili kurahisisha utekelezaji;
(d) Kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara ili kuchochea uwekezaji, hususan wa viwanda; na
(e) Kuendelea kuimarisha miundombinu wezeshi katika maeneo ya mradi.

Maelezo ya kina ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo yapo katika **Kiambatisho I.**

SURA YA TATU

VIPAUMBELE VYA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17

3.1 Malengo

Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/17 ni kuhakikisha rasilimali na fursa za nchi zinatumika vizuri ili kujenga uchumi wa viwanda na kupunguza umasikini. Malengo mahsusi ni: kuimarisha kasi ya ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kuwa ukuaji huo unanufaisha wananchi walio wengi; kuongeza mauzo nje ya bidhaa za viwandani; kuongeza fursa za ajira, hususan kwa vijana; kulinda hifadhi ya mazingira; na kusimamia utekelezaji wa mpango huu kwa nguvu zote. Vile vile, mafanikio katika ujenzi wa uchumi wa viwanda yatatakiwa yajidhihirishe katika kuongezeka kwa upatikanaji na ubora wa huduma za jamii, na kupiga hatua za kuridhisha katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

3.2 Vipaumbele

Vipaumbele vya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 vimezingatia: Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 – 2025/26); Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; na taarifa ya awali ya maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21).

3.2.1 Viwanda vya Kuimarisha kasi ya Ukuaji wa Uchumi

(a) Viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini au nguvu kazi zaidi kama vile viwanda vya kusindika na kuongeza thamani mazao ya kilimo, mifugo, misitu, na uvuvi na viwanda vya kuchakata madini;

(b) Viwanda vya kuzalisha bidhaa ambazo zinatumiwa na watu wengi nchini hususan nguo, viatu, mafuta ya kupikia;

(c) Viwanda vinavyotumia teknolojia ya kati na kuajiri watu wengi;

(d) Viwanda kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa kukidhi mahitaji ya miji kama vile vyakula, samani, vifaa vya ujenzi, madawa, vipodozi na urembo, na viwanda vya kuunganisha magari, kompyuta na vifaa vingine vya kielektroniki;

(e) Viwanda vitakavyotumia vema fursa ya kijiografia ya Tanzania;

(f) Viwanda vya kati na viwanda mama vitakavyotumia malighafi za chuma, makaa ya mawe, magadi soda, na bidhaa za petroli na gesi; na

(g) Viwanda na TEHAMA vitakavyochochea kuongezeka kwa tija na ubunifu katika sekta mbalimbali na matumizi ya teknolojia.

3.2.2 Miradi Mikubwa ya Kielelezo (*flagship projects*)

(a) Uendelezaji wa maeneo maalum ya uwekezaji Bagamoyo, Kigoma na Mtwara;
(b) Uanzishaji wa kituo cha biashara na huduma Kurasini;
(c) Uanzishaji wa mji mpya wa kilimo Mkulazi (*Agriculture City*);
(d) Ujenzi wa kiwanda cha chuma cha Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma;
(e) Ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha kimataifa cha *standard gauge*; na
(f) Kusomesha vijana wengi kwa mkupuo katika fani za mafuta na gesi, uhandisi, kemikali, viwanda vya kioo na afya.

3.2.3 Maeneo Wezeshi kwa Maendeleo ya Viwanda

3.2.3.1 Nishati

Lengo ni kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya umeme mijini na vijijiji, maeneo ya kipaumbele ni:

(a) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya umeme ya kitaifa iliyoibuliwa katika Programu ya Matokeo Makubwa Sasa;
(b) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini na Makao Makuu ya Wilaya;
(c) Kuanza uzalishaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Kiwira (MW 200); na
(d) Kujenga miundombinu ya usambazaji gesi asilia katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Dar es Salaam.

3.2.3.2 Ardhi, Nyumba na Makazi

Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda na kilimo cha kibiashara, ambapo kipaumbele ni:

(a) Upimaji na utoaji hatimiliki za ardhi na uthamini wa majengo katika miji na majiji;
(b) Kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi;
(c) Kuandaa Mipango Kabambe (Master Plans) ya Miji, Majiji na Vijiji kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kwa lengo la kuainisha matumizi mbalimbali ya ardhi ikiwemo maeneo yatakayofaa kuanzisha viwanda na yatakayowezesha kuvipatia viwanda malighafi muhimu; na

(d) Kutambua, maeneo ya ardhi kwa lengo la kuyaingiza kwenye Hazina ya Ardhi (Land Bank).

3.2.3.3 Kilimo

Lengo ni kuhakikisha uwepo wa chakula cha kutosha na upatikanaji wa uhakika wa malighafi za uzalishaji katika viwanda vya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Maeneo ya kipaumbele ni:-

(a) **Kilimo cha Mazao**

(i) Kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ili kupunguza utegemezi wa mvua kwa kuongeza eneo la umwagiliaji hususan mazao ya mahindi, mpunga na miwa;
(ii) Kuboresha mfumo wa utafiti wa kilimo nchini na kuhakikisha matokeo ya tafiti hizo yanawafikia wakulima;
(iii) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa maghala ya kuhifadhia nafaka;
(iv) Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji;
(v) Kuimarisha mafunzo ya kilimo na huduma za ugani;
(vi) Kuwawezesha wakulima hususan vijana na wanawake kujishughulisha katika kilimo biashara;
(vii) Kuimarisha maendeleo ya ushirika nchini; na
(viii) Kuendelea kutenga, kupima na kumilikisha maeneo ya kilimo cha mazo nchini.

(b) **Mifugo**

(i) Kuongeza uzalishaji wa mitamba na kuimarisha vituo vya uhamilishaji;
(ii) Kujenga na kuimarisha miundombinu ya mifugo (malambo, visima, mabwawa, majosho na minada) katika mikoa yenye mifugo mingi;
(iii) Kuendelea kutenga, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya ufugaji nchini; na
(iv) Kuongeza udahili wa maafisa ugani na kuanzisha mashamba darasa ya malisho.

(c) **Uvuvi**

(i) Kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga bandari ya uvuvi, mialo, bandari za kutengeneza boti na vituo vya udhibiti

wa ubora na viwango;

(ii) Kuendelea kuimarisha vituo vya mafunzo na tafiti za uvuvi ili kuongeza uzalishaji wa samaki na huduma za ugani kwa wafugaji;

(iii) Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za uvuvi; na

(iv) Kuendelea kuimarisha hifadhi za bahari, maziwa makuu na maeneo tengefu.

3.2.3.4 Miundombinu

Lengo ni kuendeleza miradi ya ujenzi/ukarabati wa miundombinu ya reli, barabara, madaraja, vivuko, bandari, viwanja vya ndege, na mkongo wa Taifa wa mawasiliano iliyoanza katika kipindi cha Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano na mahususi kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya viwanda. Maeneo hayo ni:-

(a) Usafiri na Usafirishaji

Reli

(i) Kukarabati reli ya kati, hususan miradi iliyoainishwa katika programu ya Matokeo Makubwa Sasa;

(ii) Kuboresha miundombinu ya reli ya TAZARA kwa kukarabati karakana, mtambo wa kuzalisha kokoto na kuboresha vituo vya abiria;

(iii) Ujenzi wa mtandao wa reli unaounganisha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(iv) Kukamilisha taratibu za kujenga reli mpya zifuatazo: reli ya Mtwara – Mbambabay na michepuko ya kwenda Liganga na Mchuchuma; reli mpya ya Tanga – Arusha – Musoma na michepuko ya kwenda Minjingu na Engaruka; na

(v) Kuboresha usafiri wa reli jijini Dar es Salaam na kuanza utafiti wa njia mpya za reli kwa maeneo ya Bunju/Kerege, Kibaha, Chamazi na Pugu.

Barabara

(i) Ukarabati wa barabara zote zinazoendelea (km 517.2) na ujenzi kwa kiwango cha lami ambao umekwishaanza katika barabara kuu na barabara za mikoa (km 2,439.35);

(ii) Ujenzi mpya wa barabara zenye urefu wa km 5,427 na kukarabati barabara zenye urefu wa km 1,055.12 kwa kiwango cha lami;

(iii) Upembuzi na usanifu wa kina kwa kiwango cha lami kwenye

barabara zenye urefu wa km 6,530.7; na

(iv) Barabara za kupunguza msongamano katika majiji na miji mingine mikubwa ikiwemo Arusha, Mwanza na Dar es Salaam ikijumuisha ujenzi wa awamu ya pili na ya tatu ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (km 42.6).

Madaraja

(i) Kukamilisha ujenzi wa madaraja makubwa 6 ya Kilombero (Morogoro), Sibiti (Singida), Kigamboni (Dar es Salaam), Kavuu (Katavi), Lukuledi II (Lindi), na Ruvu Chini (Pwani);

(ii) Ujenzi mpya wa madaraja 2 ya Selander (Dar es Salaam) na Wami Chini (Pwani) na ukarabati wa madaraja 5 ya Ruhuhu (Ruvuma), Momba (Rukwa), Kirumi (Mara), Magara (Manyara) na Pangani (Tanga);

(iii) Kuanza usanifu wa madaraja 3 ya Simiyu (Mwanza), Mzinga (Dar es Salaam) na Mlalakuwa (Dar es Salaam); na

(iv) Kuanza ujenzi wa barabara za juu (Flyovers) kwenye makutano ya barabara za jiji la Dar es Salaam.

Bandari

(i) Kuboresha miundombinu ya bandari hususan miradi iliyoibuliwa katika Programu ya Matokeo Makubwa Sasa;

(ii) Kuboresha miundombinu na ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kuhudumia shehena katika bandari za baharini na maziwa makuu; na

(iii) Kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa bandari mpya za Mwambani (Tanga) na Mbegani (Bagamoyo).

Usafiri wa Majini

Lengo ni kuimarisha usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo majini.

Meli

(i) Ununuzi wa meli za abiria na mizigo katika ziwa Victoria (meli 1), ziwa Tanganyika (meli 1), na ziwa Nyasa (meli 1); na

(ii) Kukarabati meli zilizosimama na zinazoendelea kutoa huduma katika ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Vivuko

(i) Ununuzi wa vivuko vipya 4 vya Kigongo – Busisi (Mwanza), Rugezi – Kisorya (Mwanza), Pangani – Bweni (Tanga) na Magogoni – Kigamboni (Dar es Salaam); na
(ii) Ukarabati wa vivuko vilivyosimama na vinavyoendelea kutoa huduma katika bahari na maziwa.

Usafiri wa anga

(i) Kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga ili kuongeza ufanisi wa viwanja vya ndege;
(ii) Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika viwanja vipya vya ndege; na
(iii) Ununuzi wa ndege mpya (2) za Shirika la Ndege la Tanzania.

(b) Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

(i) Kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupanua matumizi yake katika maeneo mbalimbali nchini na nchi jirani;
(ii) Kuendelea kuunganisha miundombinu ya mawasiliano na Serikali mtandao nchini;
(iii) Tafiti, kuendeleza miundombinu na raslimali watu ili kuharakisha maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Ugunduzi;
(iv) Kuanzisha maeneo maalum ya TEHAMA;
(v) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta.

3.2.3.5 Maendeleo ya Ujuzi Maalum

Lengo ni kuongeza upatikanaji wa rasilimali watu kwa mkupuo yenye ujuzi ili kuendana na mahitaji ya uchumi wa viwanda. Maeneo ya vipaumbele ni:

(i) Uchambuzi wa mahitaji na kutoa mafunzo katika maeneo mahususi ya gesi na mafuta, chuma, urani na udaktari;
(ii) Ukarabati, ujenzi na upanuzi miundombinu katika vyuo vya mafunzo ya afya, sayansi na teknolojia na ufundi stadi; na
(iii) Uandaaji na usimamiaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Stadi za Kazi ili kuiwezesha Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kipato cha kati.

3.2.3.6 Huduma za Fedha, Biashara na Masoko

Lengo ni kuwezesha wananchi kupata mitaji ya kuwekeza na kufanya biashara ambapo vipaumbele vinavyopendekezwa ni:-

(a) Huduma za Fedha

(i) Kuongeza mtaji wa Benki ya Rasilimali Tanzania, Benki ya Wanawake na Benki ya Kilimo ili kupanua wigo wa kutoa huduma nchini kote;

(ii) Kuweka mfumo wa kuvitambua, kuvisajili na kuviwezesha vikundi vyote vyenye mwelekeo wa ushirika na ujasiriamali;

(iii) Kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini ili kuvutia uwekezaji wa taasisi za fedha nchini; na

(iv) Kuanzisha mfuko wa mzunguko (*Revolving Fund*) kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wajasiriamali kupitia ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS na VICOBA) katika maeneo mbalimbali nchini.

(b) Biashara na masoko

(i) Kuwezesha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi;

(ii) Kuweka mifumo itakayowezesha kupunguza mlolongo wa kodi, leseni na vibali visivyo vya lazima katika kuandikisha biashara; na

(iii) Kuanzisha mfumo wa uratibu na usimamizi wa biashara ndogo na kati na kutenga maeneo mahsusi kwa ajili ya biashara ndogondogo.

(c) Uwezeshaji wananchi kiuchumi

(i) Urasimishaji wa shughuli za uzalishaji mali chini ya programu ya MKURABITA;

(ii) Kuimarisha mifuko ya uwezeshaji wanawake na vijana;

(iii) Kuhaulisha fedha kwa kaya maskini; na

(iv) Kuendelea kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati.

3.2.4 Kufungamanisha Maendeleo ya Viwanda na Malengo ya Maendeleo ya Watu

Nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa ziliidhinisha Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Septemba 2015. Ili kufikia malengo hayo, Mpango wa Maendeleo 2016/17 utazingatia maeneo ya vipaumbele

yaliyoainishwa katika malengo hayo ikiwemo kuondoa umaskini, kuhakikisha usalama wa chakula, afya na elimu bora, usimamizi na upatikanaji wa maji safi na majitaka, nishati ya uhakika, upatikanaji wa ajira, hifadhi ya jamii, usawa wa jinsia na watu wenye ulemavu, utawala bora, mipango miji na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

3.2.4.1 Elimu na Afya

(a) Elimu na Mafunzo ya Ufundi

(i) Kuimarisha uwezo wa kila Sekta kuandaa mipango ya maendeleo ya rasilimali watu na kuchambua mahitaji ya ujuzi;

(ii) Ukarabati, upanuzi na ujenzi wa vyuo vikuu, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi stadi, vyuo vya maendeleo ya wananchi na vyuo vya maendeleo ya jamii;

(iii) Kuimarisha majengo na miundombinu mingine katika shule za awali, msingi na sekondari ikiwemo maabara na kuhakikisha kuwa elimu hiyo inatolewa bila malipo;

(iv) Kuongeza ubora wa elimu kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa walimu walio kazini, kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji, kuandaa mfumo endelevu wa ugharamiaji; kuimarisha mifumo ya ithibati (Accredition) na Udhibiti (inspection control);

(v) Kuimarisha mfumo, miundo na taratibu nyumbufu za kumuwezesha Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali katika mikondo ya kitaaluma na kitaalam; na

(vi) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaopata mikopo.

(b) Afya na Ustawi wa Jamii

(i) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hospitali, vituo vya afya na zahanati katika mikoa na wilaya nchini;

(ii) Kuimarisha huduma za kinga na matibabu na upatikanaji wa vifaa tiba katika hospitali za rufaa (kitaifa na kikanda) na hospitali maalum;

(iii) Kuboresha upatikanaji wa dawa na kuimarisha mfumo wa upatikanaji wake kwa wananchi;

(iv) Kuimarisha utekelezaji wa programu za kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto;

(v) Kuunganisha hospitali za rufaa za mikoa na wilaya kwenye

mifumo ya matibabu mtandao, ukusanyaji na utoaji taarifa za afya ili kuimarisha huduma;

(vi) Kuboresha huduma za matibabu nchini ili kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi;

(vii) Kujenga nyumba za watumishi wa sekta ya afya karibu na vituo vya kutolea huduma; na

(viii) Kukarabati, kujenga na kupanua miundombinu katika vyuo vya mafunzo ya afya kwa kushirikisha sekta binafsi.

3.2.4.2 Maji Safi na Majitaka

(i) Kuendelea na miradi ya maji vijijini;

(ii) Upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji mijini;

(iii) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na maji taka katika jiji la Dar es Salaam na miji mingine mikubwa;

(iv) Kuendelea na miradi mikubwa 7 ya kitaifa ya maji ya Chalinze (Pwani), Mugango - Kiabakari (Mara), Makonde (Mtwara), Handeni (Tanga), Wanging'ombe (Njombe), Masasi – Nachingwea (Mtwara) na Maswa (Simiyu); na

(v) Kuimarisha taasisi za usimamizi wa rasilimali za maji.

3.2.4.3 Kazi na Ajira

(i) Kuendelea na programu ya kukuza ajira kwa vijana awamu ya kwanza inayotekelezwa kwa miaka mitatu 2014/15 - 2016/17;

(ii) Kuendelea na programu ya kukuza ujuzi; na

(iii) Kuendesha utafiti wa kitaifa wa hali ya rasilimali watu ili kuwezesha nchi kuweka na kutekeleza mipango sahihi ya matumizi ya rasilimali watu.

3.2.4.4 Mazingira na mabadiliko ya tabia nchi

(i) Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa athari za mazingira kwa miradi mikubwa hususan viwanda na miundombinu;

(ii) Kuendeleza mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi; na

(iii) Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Uharibifu wa Mazingira.

3.2.4.5 Mipango Miji

(i) Kuandaa mipango ya miji, majiji na vijiji kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji kwa lengo la kufanya miji na makazi ya

watu yawe salama, jumuishi, himilivu na endelevu;

(ii) Kuhimiza ujenzi wa miji ya pembezoni (satelite cities) katika jiji la Dar es Salaam pamoja na miji mingine;

(iii) Kupima na kurasimisha makazi yasiyopimwa hususan kakika miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na Morogoro; na

(iv) Usimamizi endelevu wa ukuaji wa miji na majiji.

3.2.5 Maeneo Mengine Muhimu kwa ukuaji wa Uchumi na Ustawi wa Taifa

3.2.5.1 Utalii

(i) Kushirikisha sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu ya utalii;

(ii) Kuwekeza na kuendelezaji maeneo mengine yenye fursa za utalii;

(iii) Kutekeleza mkakati wa kitaifa wa utangazaji wa utalii ili kuwavutia watalii wengi zaidi;

(iv) Kutoa mafunzo ya ukufunzi katika chuo cha Taifa cha utalii kwa lengo la kuimarisha mafunzo ya utalii; na

(v) Kutenga maeneo maalum ya utalii, hususan ya fukwe za bahari na maziwa kwa ajili ya hoteli za kitalii.

3.2.5.2 Misitu na Wanyamapori

(i) Kuongeza eneo la kupanda miti na kuhakikisha kwamba mbao zinazovunwa zinatumika kutengeneza samani badala ya kusafirisha magogo nje ya nchi;

(ii) Kuboresha miundombinu na kununua vitendea kazi kwa maendeleo ya misitu na kupambana na ujangili; na

(iii) Kuimarisha usimamizi wa ikolojia, kuanzisha miradi ya kupanda miti na kuratibu mpango wa matumizi bora ya ardhi.

3.2.5.3 Madini

(i) Kuimarisha mfumo wa kukagua shughuli za migodi ili kuwepo na usimamizi endelevu wa rasilimali za madini;

(ii) Kuimarisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili liweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji na utoaji huduma katika sekta ya madini;

(iii) Kuimarisha miundombinu ya Chuo cha Madini Dodoma na Ofisi za Madini mikoani;

(iv) Kuvutia mitaji na teknolojia katika Sekta ya Madini ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Sekta na mchango wake kwenye uchumi;
(v) Kuimarisha Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania ili kuongeza ufanisi katika shughuli za ukaguzi na kusimamia uzalishaji na biashara ya madini nchini; na
(vi) Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini ili kuongeza mapato na ajira.

3.2.5.4 Hali ya hewa

(i) Kuimarisha uwezo na miundombinu ya mamlaka ya hali ya hewa kwa kuongeza matumizi ya vifaa vya kisasa; na
(ii) Ununuzi wa rada za hali ya hewa.

3.2.5.5 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

(i) Kujenga, kukarabati na kununua majengo kwa ajili ya balozi za Tanzania;
(ii) Kuboresha mfumo wa mawasiliano kati ya Serikali na balozi zake nje ya nchi; na
(iii) Kukamilisha vituo vya utoaji huduma kwa pamoja mipakani.

3.2.5.6 Utawala Bora

(i) Kuimarisha miundombinu na vitendea kazi katika taasisi zinazosimamia utawala bora (TAKUKURU, Mahakama, Tume ya Maadili, Bunge, na Ulinzi na Usalama);
(ii) Kutekeleza mkakati wa mapambano dhidi ya rushwa awamu ya tatu;
(iii) Kuboresha sekta ya umma ili itoe huduma kwa ufanisi;
(iv) Kufanya mapitio ya sheria zinazohusu usajili wa matukio muhimu ya binadamu;
(v) Kukamilisha mchakato wa kupata katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
(vi) Kuimarisha mfumo wa Kujitathmini Kiutawala Bora - APRM; na
(vii) Kuharakisha upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa.

SURA YA NNE

UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17

4.1 Utangulizi

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17 utagharamiwa na Serikali kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani, misaada na mikopo, Sekta Binafsi na ubia kati ya sekta ya Umma na Binafsi. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hususan sekta binafsi itahakikisha rasilimali watu na fedha zinapatikana kutekeleza Mpango. Aidha, msisitizo utawekwa katika kutenga bajeti na kulinda fedha za kutekeleza miradi mikubwa ya kielelezo iliyoainishwa katika Mpango.

4.2 Ugharamiaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16)

Makadirio ya bajeti ya kutekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 - 2015/16) yalikuwa shilingi trilioni 44.5 ambayo ni wastani wa shilingi trilioni 8.9 kila mwaka. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 2.9 zilitarajiwa kuwa fedha za ndani na shilingi trilioni 6.0 sekta binafsi na washirika wa maendeleo. Katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango huo, fedha za ndani zilizotolewa zilifikia wastani wa shilingi trilioni 2.9 kwa mwaka. Aidha, katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, fedha za maendeleo zilizotolewa ni wastani wa asilimia 26 ya bajeti halisi kwa mwaka ikilinganishwa na lengo la asilimia 35. Kwa upande wa mchango wa sekta binafsi na washirika wa maendeleo haukufikia asilimia 50 kutokana na ushiriki mdogo wa sekta binafsi na wafadhili kutotimiza ahadi zao. **Kielelezo Na. 4.1** kinaeleza mwenendo wa ugharamiaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Kielelezo Na 4.1: Mwenendo wa Ugharamiaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 -2015/16)

	Mwaka	Makadirio ya FYDP I (Sh. Mil.)	Bajeti Halisi ya Serikali (Sh. Mil.)	Fedha za Maendeleo Ndani na Nje (Sh. Mil.)	Fedha za Maendeleo za Ndani (Sh. Mil.)	Fedha za Maendeleo za Nje (TSh Mil)	Fedha za Maendeleo za Ndani na nje /Bajeti Halisi ya Serikali (%)
Matumizi Halisi	2010/11	-	10,202,602	2,749,037	984,555	1,764,482	27%
	2011/12	8,473,812	12,171,877	3,774,722	1,872,312	1,902,410	31%
	2012/13	11,878,988	14,162,228	3,844,291	2,277,553	1,566,738	27%
	2013/14	9,917,372	15,667,535	3,926,043	2,121,212	1,804,831	25%

	Mwaka	Makadirio ya FYDP I (Sh. Mil.)	Bajeti Halisi ya Serikali (Sh. Mil.)	Fedha za Maendeleo Ndani na Nje (Sh. Mil.)	Fedha za Maendeleo za Ndani (Sh. Mil.)	Fedha za Maendeleo za Nje (TSh Mil)	Fedha za Maendeleo za Ndani na nje /Bajeti Halisi ya Serikali (%)
	2014/15	7,901,872	16,637,765	3,452,855	2,264,506	1,188,349	21%
Makadirio ya Matumizi	2015/16	6,314,743	22,495,492	5,919,054	4,256,873	1,662,181	26%

Chanzo: Wizara ya Fedha, 2015.

Angalizo: Bajeti halisi ya Serikali inajumuisha fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo.

4.3 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2015/16

Katika mwaka 2015/16, Serikali ilitenga shilingi 5,906,953,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi 4,244,772,439,000 na fedha za nje ni shilingi 1,662,180,561,000. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ni shilingi 739,350,941,000 ambapo fedha za ndani ni shilingi 595,000,000,000 na fedha za nje ni shilingi 144,350,941,000. Kwa upande wa Wizara, Taasisi, Wakala na Idara zinazojitegemea zilitengewa shilingi 5,167,602,059,00 ambapo fedha za ndani ni shilingi 3,649,772,439,000 na fedha za nje ni shilingi 1,517,829,620,000.

Fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa hadi Desemba 2015 ni shilingi 1,845,568,087,319, kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi 1,619,546,746,000 na fedha za nje ni shilingi 226,021,341,319. Kati ya fedha zote zilizotolewa, shilingi 1,745,831,824,337 ni kwa ajili ya Wizara na Taasisi za Serikali ambapo fedha za ndani ni shilingi 1,619,196,746,000 na fedha za nje ni shilingi 126,635,078,337. Kwa upande wa Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri, jumla ya fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa ni shilingi 99,736,262,982 ambapo fedha za ndani ni shillingi 350,000,000 na fedha za nje ni shillingi 99,386,262,982. Katika kipindi kinachoishia Desemba 2015, fedha za maendeleo zilizotolewa ni sawa na asilimia 31.2 ya fedha zote za maendeleo. Fedha za ndani zilizotolewa ni sawa na asilimia 38.2 ya bajeti ya fedha za ndani na fedha za nje zilizotolewa ni sawa na asilimia 13.6 ya bajeti ya fedha za nje. Hali hii ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika kipindi hiki imesababisha kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

4.4 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2016/17

Katika mwaka 2016/17, makadirio ya bajeti ya maendeleo ni shilingi bilioni 5,899.9 ambapo fedha za ndani shilingi bilioni 4,527.8 sawa na asilimia 76.7

ya fedha za maendeleo na fedha za nje ni shilingi bilioni 1,372.1. Fedha hizo zitatokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo mapato ya ndani, mapato ya nje, ubia kati ya sekta ya umma na binafsi na uwekezaji wa sekta binafsi na mikopo nafuu hususan kutoka katika taasisi za benki za hapa nchini ikiwemo TIB na TADB. Matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa asilimia 6.7 ya Pato la Taifa katika mwaka 2016/17. Aidha, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 itawezesha utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa ufanisi.

4.5 Vyanzo vya Mapato ya Ndani

Katika mwaka 2016/17, Serikali itagharamia miradi ya maendeleo kupitia vyanzo vya ndani vya mapato vilivyopo vikiwemo vya Halmashauri, vyanzo vipya vilivyopendekezwa katika maabara ya ukusanyaji wa mapato, ambavyo ni kodi, mapato yasiyo ya kodi, misaada na mikopo, dhamana za mikopo na vyanzo vingine vya mapato ya ndani. Vile vile, Serikali itaendelea kukopa ndani ya nchi kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia ukomo wa kukopa ndani ya nchi usiozidi asilimia 1 ya Pato la Taifa. Serikali inatarajia kukusanya mapato ya ndani ambayo ni asilimia 16.9 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2016/17.

4.6 Vyanzo vya Mapato ya Nje

Taarifa ya Uchambuzi ya Uhimilivu wa Madeni ya mwaka 2015 (Debt Sustainability Analysis) iliyoandaliwa na Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inaonesha kuwa deni la Taifa linahimilika, hivyo Tanzania itaendelea kukopa mikopo yenye masharti nafuu na kutumia misaada inayotolewa na washirika wa maendeleo kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vile vile, katika mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara ili kufanikisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya miundombinu. Katika mwaka 2016/17, Serikali imepanga kukopa kiasi cha dola za Kimarekani milioni 800. Aidha, Serikali itaendelea kutumia vyanzo mbalimbali kama hati fungani za miundombinu na akiba, makubaliano ya ushirikiano wa kiuchumi kikanda, hati fungani maalum na kuzingatia ukomo wa uhimilivu wa deni la Taifa katika mchakato wa kukopa fedha nje ya nchi.

4.7 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Katika mwaka 2016/17, idadi ya miradi itakayotekelezwa chini ya ubia wa Serikali na Sekta Binafsi (PPP) inatarajiwa kuongezeka kufuatia kukamilika kwa sera, sheria na kanuni za PPP. Kupitia utekelezaji wa PPP, Serikali itapata

nafuu katika bajeti ya maendeleo hususan katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu na hivyo kuongeza wigo wa kutekeleza maeneo mengine ya Mpango wa Maendeleo. Serikali itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wadau wa sekta binafsi ili washiriki kikamilifu katika uwekezaji kwa ubia na sekta ya umma.

4.8 Uwekezaji wa Sekta Binafsi

Utekelezaji wa viwanda nchini kwa kiwango kikubwa utategemea ushiriki wa sekta binafsi. Hivyo, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kupanga mikakati ya kushawishi sekta binafsi ya ndani na nje ya nchi kushiriki kuibua na kutekeleza Mpango, kulea utamaduni wa uadilifu na uwajibikaji wa kijamii, kutoa muongozo na taratibu za sekta binafsi kushiriki katika miradi kwa njia ya ubia na sekta ya umma na kuweka mikakati ya kuvutia uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja.

4.9 Mikopo Nafuu kutoka Taasisi za Benki za Nchini.

Kwa kutambua changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa mitaji ya uwekezaji unaochukua muda mrefu, ipo haja ya kusaidia taasisi za fedha za kimaendeleo (DFIs) za ndani, ikiwa ni pamoja na kuzipa nafasi ya kipekee katika kubainisha mikakati muafaka ya kukusanya na kugharamia uwekezaji mkubwa na wa muda mrefu wa miradi ya maendeleo.

SURA YA TANO

UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

5.1 Utangulizi

Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17 utazingatia mfumo na mwongozo utakaotumika katika ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo. Mfumo huo wa ufuatiliaji na tathmini utatekelezwa kwa kuweka malengo ya utekelezaji kwa kila sekta kwa mwaka na kuandaa mpango kazi wa mwaka. Utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo utazingatia mwongozo wa Mpango na bajeti, na mwongozo wa uandaaji na usimamizi wa miradi ya umma *(Public Investment Management – Operational Manual).* Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha idara za ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ili miradi iliyoanzishwa iweze kuleta tija kwa Taifa.

5.2 Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo

5.2.1 Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa

Katika mwaka 2015/16, utekelezaji wa miradi ya Matokeo Makubwa Sasa ulifuatiliwa kwa kushirikiana na Vitengo Maalum vya Ufuatiliaji vya Wizara. Sekta zilizofuatiliwa ni Kilimo, Viwanda, Elimu, Uchukuzi, Maji, Nishati, na Fedha. Taarifa za ufuatiliaji wa Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa zinazingatia maeneo ya kipaumbele kupitia viashiria vilivyowekwa katika kila sekta.

5.2.2 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati

Katika robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2015/16, Wizara ya Fedha na Mipango ilifuatilia miradi ya maendeleo 38 katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Geita, Iringa, Mbeya, Kagera, Morogoro, Mwanza, Singida, Shinyanga, Simiyu na Tabora. Miradi iliyofuatiliwa ilijumuisha ya Umma na Sekta Binafsi, katika maeneo ya viwanda, barabara, bandari, viwanja vya ndege, nishati, maji, umwagiliaji, mifugo, viwanda, afya na mkongo wa Taifa.

(a) Barabara

Barabara za Isaka - Lusahunga (km 242), Lusahunga - Rusumo (km 90), Iringa - Dodoma (km 259.6) na Manyoni - Itigi (km 70.9): Kwa upande wa barabara ya Isaka - Lusahunga, ukarabati wa barabara eneo la Isaka - Ushirombo na ujenzi wa miundombinu ya madaraja umekamilika. Aidha,

ukarabati wa barabara ya Ushirombo - Lusahunga (km 40) umesimama kutokana na madai ya Mkandarasi ambaye amelazimika kuondoa vifaa eneo la mradi. Kwa upande wa barabara ya Lusahunga - Rusumo, ukarabati wa maeneo yaliyoharibika unaendelea ili kupunguza usumbufu wa watumiaji wa barabara hii ambayo ina mashimo mengi. Kwa upande wa barabara za Iringa - Dodoma na Manyoni - Itigi ujenzi umekamilika lakini kuna uharibifu mkubwa wa barabara unaofanywa na wananchi. Mkandarasi anaendelea na taratibu za kukamilisha uwekaji wa alama za barabarani.

(b) Reli

Reli ya Kati eneo la Kitaraka na Malongwe (km 89): Kazi ya kutandika reli ya ratili 80 kwa yadi ipo katika hatua za mwisho. Hata hivyo, utaratibu wa matengenezo ya mara kwa mara wa reli bado ni changamoto kwa kuwa usimamizi wa reli unaratibiwa kwa kiwango kikubwa makao makuu na hivyo kupunguza ufanisi wa kazi. **Reli ya Kati ya Isaka – Buhongwa – Mwanza:** Utekelezaji wa mradi huu bado haujaanza kutokana na ukosefu wa fedha.

(c) Bandari

i) **Bandari ya Bukoba:** Miundombinu ya kuhudumia meli bandarini ni chakavu na haitoshelezi. Aidha, bandari imezungukwa na gati za watu binafsi ambao wamevamia eneo la bandari na kuleta ushindani. Ufanisi wa bandari umeathiriwa kwa sababu ya kusuasua kwa usafirishaji kwa njia ya reli ya kati na kukosekana kwa meli za kutosha za abiria na mizigo katika ziwa Victoria.

ii) **Bandari ya Nansio-Ukerewe**: Bandari hii inahudumia wastani abiria 3,800 (Inwards), abiria 5,000 (outwards) na wastani wa mizigo tani 75 (inwards) na tani 25 (outwards). Eneo la bandari lilipanuliwa mwaka 2014 baada ya ununuzi na ulipaji fidia kwa upande wa mashariki mwa bandari ya Nansio na kufikia hekta 2. Kuanzia mwaka 2006 Bandari ya Nansio ilikuwa chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) ambapo kulikuwa na meli mbili (2) zilizokuwa zikitoa huduma asubuhi na mchana lakini kwa sasa meli ya Serikali moja imeharibika, hivyo imebaki meli moja tu ya kampuni binafsi ya MV Nyehunge inayotoa huduma mara moja kila siku. Baadhi ya majengo ya kisasa yamejengwa likiwemo jengo la ofisi ya kisasa, chumba cha mapumziko ya abiria, chumba cha wageni maalum yaani V.I.P na sehemu ya mgahawa. Bandari hii inahitaji maboresho makubwa ya gati na eneo la bandari ya Nansio. Aidha, zinahitajika meli 2 zaidi kwa kuwa mahitaji ya usafiri wa mizigo na abiria kati ya Mwanza na

Ukerewe ni makubwa sana. Hata hivyo, kuna umuhimu wa kuwa na bandari katika eneo la Ngoma/Kisorya (Ukerewe – Bunda) kwa kuweka gati pande zote mbili na kuongeza kivuko cha pili ili kuimarisha usafiri kati ya Ukerewe, Bunda na maeneo mengine ya nchi.

(d) Viwanja vya Ndege:

i. **Kiwanja cha Ndege cha Songwe:** Songwe ni kiwanja kipya cha ndege kilichopo Mbeya. Upembuzi yakinifu wa kiwanja hiki ulifanyika mwaka 1988 na usanifu wa kina ulifanyika mwaka 1997 ambapo usanifu wa kina ulikuwa ni kwa ajili ya ndege aina ya Fokker 50. Aidha, kutokana na maendeleo ya kiuchumi na kijamii Serikali iliamua kupanua miundombinu ya kiwanja ili kukidhi matumizi ya ndege kubwa zinazolingana na ukubwa wa Boeing 737 zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 100 badala ya ndege ndogo zilizoainishwa kwenye usanifu wa awali. Ujenzi wa kiwanja ulianza mwaka 2001 na ilipofika mwaka 2012 kiwanja kilifunguliwa kwa ajili ya matumizi. Ujenzi wa jengo jipya la abiria ulianza mwaka 2013 na unategema kuisha kabla ya Juni, 2016. Ujenzi wa jengo hilo ukikamilika uwanja utakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 250,000 kwa mwaka. Changamoto za kiwanja ni pamoja na: kukosekana kwa uzio wa kiwanja; na kutokuwa na *navigational aids* ikiwemo taa katika njia za kutua na kurukia ndege. Eneo la Mbeya (Songwe) kuwa na ukungu hususan wakati wa asubuhi na hivyo kuwa vigumu kwa marubani wa ndege kuona kiwanja vizuri.

(e) Nishati

i) Miradi ya Kuzalisha Umeme

Bwawa la Mtera: Uzalishaji wa umeme katika bwawa si wa kuridhisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya hali ya hewa, kilimo cha umwagiliaji, ufugaji holela, uchakavu wa mitambo na upotevu wa maji. Aidha, kukamilika kwa barabara ya Iringa – Dodoma kumeongeza idadi ya magari yanayopita katika daraja la mto Mtera na hivyo kutishia uhai wa daraja na bwawa. **Mradi wa Umeme wa Upepo Singida:** Katika eneo la mradi kimejengwa kituo cha kupima kasi ya upepo ambacho kimewezesha kubaini uwezo wa kuzalisha umeme MW 100. Aidha, umeme utakaozalishwa utaunganishwa kwenye gridi ya Taifa Singida mjini. Mradi unategemea kuanza baada ya kupatikana mkopo wa dola za

Kimarekani milioni 136 kutoka benki ya Exim ya China. **Mradi wa Umeme Rusumo:** Utekelezaji wa mradi huu bado haujaanza. Hata hivyo, makubaliano baina ya Tanzania, Rwanda na Burundi yamesainiwa ambapo kila nchi itapata MW 27. Kwa upande wa Tanzania umeme utaunganishwa kwenye gridi ya Taifa baada ya kukamilika mradi wa kusafirisha umeme kV 220 wa Geita – Nyakanazi. **Kituo cha kuzalisha umeme wa maji Kidatu:** Kituo kina uwezo wa kuzalisha MW 204 katika bwawa lenye mita za ujazo wa 125. Shughuli zilizotekelezwa katika kipindi husika ni pamoja na kufunga mitambo mipya ya kupozea hewa, Kuondoa kinyesi cha popo toka kwenye shimo/ handaki, ununuzi ya vali na pampu za maji ya kusafisha mitambo na pampu za maji safi na maji taka na kuendelea kubadilisha mitambo ya kukata umeme na kutenganisha umeme wa mkondo wa kV 220 katika njia ya MG1,T1 na T2. Shughuli zinazoendelea ni kubadili mfumo wa kuongozea mitambo (control system), kubadili mfumo wa upoozaji hewa ndani, kubadilisha mfumo wa DC power house na kubadilisha vidhibiti mwendo (Gavana). Changamoto zilizopo ni uchakavu wa mitambo, uhaba wa maji na fedha. Hata hivyo, kuna fursa kubwa ya kuzalisha umeme katika kituo hicho. **Kituo cha kuzalisha umeme wa maji Kihansi:** Kituo kipo kwenye bonde la mto Rufiji umbali wa kilomita 540 kutoka Dar es Salaam kwenye milima ya Udzungwa. Kituo kina uwezo wa kuzalisha Megawati 180 na mitambo mitatu (3) yenye ukubwa wa megawati 60 kila mmoja. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kubadilisha mfumo wa kuongozea mitambo (control system), kubadilisha mfumo wa upoozaji hewa ndani ya power plant, kubadilisha mfumo wa *DC power* house na kubadilisha vidhibiti mwendo (Gavana) kwenye mitambo. Changamoto zinazokabili kituo ni uchakavu wa mitambo ambayo inaongeza gharama za uendeshaji na uhaba wa fedha kwa ajili ya kufunga mashine za ziada mbili (2) ili kufikia lengo la mashine tano (5) kwa kituo.

ii) **Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira:** Mgodi huu upo mpakani mwa Wilaya za Kyela na Ileje katika Mkoa wa Mbeya. Mgodi huu ulianza 1988 kwa msaada wa Serikali ya China ukiwa na mashapo ya makaa ”economical reserve” ya tani milioni 35.14, kati ya hayo mashapo ya kisanifu (proved reserve) ni tani milioni 22.14 na mashapo yanayoweza kuvunwa kwa faida (Mineable reserve) ni tani milioni 14.64 za makaa. Awali mgodi ulilenga kuzalisha makaa ya mawe tani

150,000 kwa mwaka kwa ajili ya nishati ya matumizi ya viwanda vya hapa nchini vya Saruji (Mbeya), Karatasi cha Mgololo (Mufindi), na viwanda vya chai vya Katumba na Musekela (Tukuyu). Mgodi ulibinafsishwa mwaka 2005 kwa Kampuni ya Kiwira Coal Mines Ltd ambapo Serikali ya Tanzania ilimiliki asilimia 30 ya hisa na Tan Power Resources asilimia 70 ya hisa. Lengo kuu la mgodi kwa kipindi hiki lilikuwa ni kuzalisha makaa ya mawe tani milioni moja kwa ajili ya kuzalisha umeme.

(f) Viwanda

i) **Kiwanda cha Alizeti cha Singida Fresh Oil Mill:** Kiwanda kilianzishwa mwaka 2006 na kinamilikiwa na mtu binafsi ambapo kina uwezo wa kusindika tani 200 za alizeti kwa siku. Alizeti inayosindikwa kiwandani inanunuliwa moja kwa moja kutoka kwa wakulima. Kiwanda pia hutoa huduma ya usindikaji wa alizeti kwa wafanyabiashara wengine. Hata hivyo kiwanda bado ni kidogo na kinatumia teknolojia ya nguvu kazi nyingi zaidi (labour intensive). Kiwanda kimeajiri wafanyakazi 16 katika ajira ya masharti ya kudumu na wafanyakazi 90 kwa masharti ya ajira ya muda.

ii) **Kiwanda cha Nguo cha 21st Century – Morogoro:** Kiwanda cha 21st Century Textiles Ltd kilianzishwa mwaka 2003 baada ya kubinafsishwa kwa kiwanda cha nguo cha Morogoro Polyester Textiles Ltd. Kiwanda kilianza uzalishaji wa nguo ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani. Kiwanda kimefanya maboresho mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuondoa mitambo ya zamani na kufunga mitambo mipya inayotumia teknolojia ya kisasa na hivyo kusababisha kiwanda kuzalisha bidhaa bora zaidi kwa gharama nafuu. Kutokana na uwekezaji katika mashine na teknolojia hizo, kiwanda kina uwezo wa kuzalisha mita milioni 60 kwa mwaka ilikinganishwa na uzalishaji wa mita milioni 16 kwa mwaka kabla ya kubinafsishwa. Aidha, ufanisi wa kuhudumia wateja umeongezeka ambapo mteja anaweza kupata bidhaa aliyoagiza katika kipindi cha wiki moja. Kiwanda kimeweza kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 1,800 ikilinganishwa na ajira 1,260 kabla ya kubinafsishwa. Kiwanda pia kimeweza kutoa ajira zisizo za moja kwa moja zipatazo 10,000. Baadhi ya changamoto za kiwanda ni: uingizaji haramu wa nguo kutoka nje ambazo hazilipiwi kodi na hivyo kuuzwa kwa bei ndogo na kupelekea ushindani usio wa haki katika soko; na kukatika mara kwa mara kwa nishati ya umeme kutoka TANESCO bila taarifa na hivyo kuathiri uzalishaji na mara nyingine

uharibifu wa mitambo.

iii) **Kiwanda cha Sukari Kilombero – Morogoro:** Kiwanda hiki kilianzishwa mwaka 1962 na kubinafsishwa mwaka 1998 ambapo Serikali ya Tanzania inamiliki asilimia 25 ya hisa zote na makampuni ya Illovo Sugar asilimia 55 na ED&F Man asilimia 20. Hii imepelekea kiwanda hicho kuwa sehemu ya kampuni ya Illovo barani Afrika. Kiwanda kimewekeza zaidi ya shilingi bilioni 6.5 kwenye miradi ya huduma za jamii. Kiwanda kinatoa ajira za moja kwa moja 5,000 na kuwawezesha wananchi kati ya 80,000 na 100,000 katika bonde la mto Kilombero kujiajiri katika kilimo cha miwa. Vile vile, kiwanda kimewekeza katika kilimo cha miwa katika eneo lenye jumla ya hekta 10,000. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto ya wafanyabiashara wasio waaminifu huingiza sukari ya viwandani ikiwa na msamaha wa kodi na kuiuza kwa matumizi ya kawaida hivyo kuathiri soko la sukari nchini.

iv) **Kiwanda cha Karatasi Mufindi (Mufindi Paper Mills) – Iringa:** Kiwanda kilibinafsishwa mwaka 2004 kwa Rai Group kutoka Kenya kwa asilimia mia moja. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 60,000 za karatasi kwa mwaka na kinatumia miti aina ya pine eucalyptus na black wattle inayovunwa katika mashamba ya Serikali ya Sao Hills yaliyopo wilayani Mufindi. Kiwanda kinazalisha karatasi aina ya kaki (brown papers) zenye uzito tofauti kulingana na mahitaji ya soko la ndani na nje. Mwekezaji alifanya ukarabati mkubwa wa mashine ya karatasi na kusimika mashine mpya za kisasa na mitambo ya kufua umeme wa MW 10 ambapo uzalishaji uliongezeka hadi tani 120,000 kwa mwaka. Vile vile, kiwanda kimetoa ajira 746 za kudumu na ajira 595 za muda. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto kubwa tatu zikiwemo: magogo ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa karatasi; na mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji na wanavijiji.

v) **Kiwanda cha Saruji – Mbeya**: Kiwanda cha saruji Mbeya kilijengwa mwaka 1977 na kuanza uzalishaji mwaka 1983 chini ya usimamizi wa Serikali. Kiwanda kilibinafsishwa mwaka 2001 kwa kampuni ya Lafarge ya Switzerland ambapo Serikali inamiliki hisa asilimia 25, Lafarge asilimia 65 na NSSF asilimia 10. Hivi sasa kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 350,000 kwa mwaka ambapo kati ya hizo asilimia 90 zinauzwa katika soko la ndani na asilimia 10 zinauzwa kwa nchi jirani za Zambia, Malawi, Burundi na DRC. Kiwanda kimetoa ajira za moja kwa moja 340 ambapo na ajira 685 zitokanazo na wakandarasi wa kiwanda. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto za:

miundombinu mibovu ya usafirishaji hususan reli ya TAZARA na isiyo na uhakika; miundombinu hafifu ya kuhudumia mizigo katika bandari ya Kasanga; umeme usio wa uhakika kutoka TANESCO ambao hukatika angalau mara moja kwa siku; na bei kubwa ya makaa ya mawe kutoka TANCOAL.

vi) **Kiwanda cha nguo –Mwanza (Mwatex):** Kiwanda cha Mwatex 2001 Limited kilibinafsishwa mwaka 2001 ambapo kilifanyiwa ukarabati na kuongeza baadhi ya vitendea kazi (mashine) na kuanza uzalishaji rasmi mwaka 2003, hususan kanga, kitenge, kikoi, shuka, sare za shule, mikoba na mafuta ya chakula. Kiwanda kipo eneo la Nyakato katika jiji la Mwanza na kina eneo la ekari 44.5. Changamoto kubwa ya kiwanda ni tatizo la nishati ya umeme kutoka TANESCO, maji, pamba chafu na watumishi wenye ujuzi wa kazi za viwanda vya nguo. Kutokana na changamoto hizo, mwaka 2012 kiwanda kilipunguza idadi ya wafanyakazi kutoka 1,235 hadi 340 ikiwa ni sehemu ya kupuguza gharama za uzalishaji.

(g) Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

Mtukula Kagera: Kituo cha Mtukula kinaunganisha huduma za Mkongo wa Taifa wa mawasiliano na nchi ya Uganda. Hadi sasa kampuni ya Roke Telecom ya Uganda imeshaunganishwa na bado kuna mahitaji makubwa ya matumizi ya mkongo huo kutoka nchi jirani. Changamoto kubwa ni usimamizi na utunzaji wa miundombinu ya kituo cha mawasiliano.

(h) Kilimo

Skimu ya Umwagiliaji – Idodi (Iringa): Mradi una mifereji ya umwagiliaji 2, mfereji wa Idodi (mita 1,950) na Mbuyuni (mita 1,850). Mradi huu unalenga kuongeza tija ya uzalisha wa mpunga na utatumika kumwagilia eneo la hekta 600. Ujenzi wa mradi unaendelea na umefikia zaidi ya asilimia 85 ambapo sehemu kubwa ya ujenzi iliyokamilika ni njia kuu. Hata hivyo, usanifu wa skimu ya umwagiliaji wa eneo la mradi haujazingatia njia za michepuko na hivyo kuashiria upotevu mwingi wa maji wakati wa umwagiliaji. **Maghala ya COWABAMA – Iringa:** Ujenzi wa ghala lililopo kijiji cha Ibangamoyo kata ya Ulanda upo katika hatua za mwisho kukamilika. Hata hivyo, ujenzi wa ghala una changamoto ya nyufa kabla kuanza kutumika. Aidha, ghala linaonekana kutotosheleza mahitaji ya wakulima wa eneo hilo.

(i) Mifugo

Shamba la Kitengule - Kagera: shamba hili linamilikiwa na Kampuni ya Kagera Sugar na lina ukubwa wa hekta 28,000 ambapo hekta 14,000 ni kwa shughuli za ufugaji na hekta 14,000 kilimo cha miwa. Shamba lina jumla ya ng'ombe 257 kwa ajili ya biashara ya nyama. **Shamba la Misenyi – Kagera**: Shamba linamilikiwa na NARCO na lina ukubwa wa hekta 23,998. Shamba lina jumla ya ng'ombe 8,000 kwa ajili ya biashara ya nyama. Changamoto kubwa ya mashamba ya mifugo ni magonjwa, upatikanaji wa chanjo, madawa na vyakula vya mifugo.

(j) Uvuvi

Kituo cha Ufugaji Samaki cha Kingolwira Morogoro kwa sasa kinazalisha na kusambaza mbegu bora za samaki na kutoa elimu ya ugani juu ya ufugaji bora wa samaki. Kituo kina matanki 21 kwa ajili ya shughuli za utafiti pamoja na kukuzia vifaranga wa perege na kambale. Ujenzi wa maabara ya sehemu ya kuzalishia vifaranga vya samaki ipo katika hatua za mwisho. Kituo kina mabwawa 12 ya kuchimba yenye ukubwa wa mita 10 kwa 20 lakini hayana uzio wa kuzuia viumbe waharibifu.

(k) Maji

Upanuzi wa mradi wa maji safi, Bomba Kuu la Ziwa Viktoria Sorwa upo katika hatua za maandalizi ambapo mtaalam mwelekezi anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu. Hata hivyo, miundombinu ya awali ya mradi hususan kwenye chanzo cha maji imechakaa na hivyo kutishia uendelevu wa mradi. **Mradi wa Maji wa Vijiji 10 Katika Mkoa wa Kagera** unatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya zote za Kagera pamoja na Manispaa ya Bukoba. Miradi iliyotembelewa ni ile inayotekelezwa katika mitaa ya Manispaa ya Bukoba ambayo ni Rwazi, Bunkago, Bushaga na Ihyoro. Sehemu kubwa ya miradi hii hutumia pampu kwa ajili ya kuvuta maji kutoka vyanzo vya maji 4 kwenda kwenye matanki 4. Mradi wa vijiji 10 ulikamilika kwa asilimia 100 katika maeneo ya Kagandokaluguru, Kyamuzinga, Ijuganyondo (A & B), Bunkago, Rwazi, Bulibata na Kyamyosi na mitaa mingine ipo katika hatua mbalimbali. **Mradi wa vijiji kumi katika Mkoa wa Shinyanga** unafadhiliwa na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na wananchi. Mkoa wa Shinyanga uliazimia kutekeleza miradi 47, miradi 26 imekamilika, 15 inatekelezwa na 6 imesimama. Miradi hiyo ipo katika maeneo ya Mwagala - Manispaa ya Shinyanga, Bushola-Manispaa ya Shinyanga, Didia - Shinyanga Vijijini, Nyashimbi - Shinyanga Vijijini, Bunambiyu – Kishapu na Mwigumbi - Kishapu. Changamoto kubwa katika uendeshaji wa miradi hii ni pamoja na

mwamko mdogo wa kufuatilia mapato na matumizi ya mradi kutoka kwa wanakijiji, kamati za maji na wahasibu kutojengewa uwezo ipasavyo juu ya namna ya usimamizi na utunzaji fedha za mradi wa maji. **Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Maji Mwanjoro** uliopo Wilaya ya Meatu, Simiyu unasuasua kutokana na changamoto ya fedha na usimamizi. Kwa sasa mkandarasi amesimamisha ujenzi na kuondoa vifaa eneo la mradi.

(l) Vituo vya Utoaji Huduma za Pamoja Mpakani

Rusumo na Mtukula: Ujenzi wa majengo ya vituo vya utoaji huduma kwa pamoja mpakani vimekamilika na vimeanza kutumika. Hata hivyo, vituo vyote bado vinakabiliwa na mahitaji muhimu ya kuendesha shughuli za wadau waliomo katika majengo hayo, ikiwemo huduma za benki na TEHAMA. Kwa upande wa Mtukula miundombinu muhimu zaidi haikuzingatiwa ikiwemo maegesho na kituo cha kuhifadhi mizigo.

5.2.3 Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa

Katika ufuatliaji wa miradi hiyo zilijitokeza changamoto zifuatazo:

i. Upatikanaji wa fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
ii. Hatimiliki za maeneo ya baadhi ya miradi hususan miradi ya bandari;
iii. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kutozingatia hali halisi ya eneo kwa baadhi ya miradi mikubwa kama ujenzi wa vituo vya kutoa huduma kwa pamoja mipakani;
iv. Miundombinu wezeshi ikiwemo maji, barabara na umeme kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
v. Baadhi ya Wizara na taasisi kutekeleza miradi ambayo kimsingi ingeweza kutekelezwa na kusimamiwa katika ngazi za mikoa na halmashauri hususan miradi ya maji, mifugo na uvuvi;
vi. Ushiriki wa sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
vii. Ukosefu wa nishati ya umeme wa uhakika na hivyo kupunguza uzalishaji katika viwanda;
viii. Ushindani mkubwa kutoka nchi zinazozalisha bidhaa ambazo huzalishwa ndani.

Katika kukabiliana na changamoto zilizobainishwa, Serikali inakusudia:

i. Kuimarisha vyanzo vya mapato vya kodi na visivyo vya kodi;
ii. Kuweka msukumo mkubwa kwa Taasisi na Wakala za Serikali kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

iii. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini ili kuimarisha uwekezaji wa sekta binafsi katika Viwanda;
iv. Kupanga mipango na bajeti ili kuwezesha miradi ya maendeleo inayotegemeana kuweza kutekelezeka;
v. Kuweka utaratibu utakaowezesha kutenga fedha za kutekeleza miradi kwa wakati uliopangwa na za kutosha;
vi. Kuhakikisha asilimia 35 ya bajeti inatengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kama ilivyokubalika; na
vii. Kulinda fedha za kutekeleza miradi ya kielelezo (*flagship projects*) ili zisitumike katika matumizi mengine.

5.3 Mgawanyo wa Majukumu

5.3.1 Wizara ya Fedha na Mipango

Wizara ya Fedha na Mipango itafuatilia na kutathmini miradi ya Kitaifa ya kimkakati na mingine muhimu kwa ukuaji wa uchumi kwa kushirikiana na Wizara, Idara, Taasisi na Wakala za Serikali. Aidha, itachambua taarifa za ufuatiliaji na tathmini na kutoa maeneo ya kuboresha utekelezaji wa miradi ya Kitaifa ya Kimkakati na Matokeo Makubwa Sasa.

5.3.2 Ofisi ya Rais – TAMISEMI

Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo itakayotekelezwa katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, itachambua taarifa za ufuatiliaji na tathmini na kutoa maeneo ya kuboresha utekelezaji wa miradi katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

5.3.3 Wizara, Idara, Taasisi na Wakala za Serikali

Wizara, Idara, Taasisi na Wakala za Serikali zina wajibu wa kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi iliyo katika maeneo yao na zinasisitizwa kuwa na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo. Aidha, Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma, 2014 umeainisha masuala ya kuzingatiwa katika ufuatiliaji na tathmini yakijumuisha upimaji wa malengo, matumizi ya rasilimali fedha kulingana na mpango kazi, changamoto, vihatarishi na ushirikishwaji wa wadau. Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya Matokeo Makubwa Sasa utaratibiwa kwa kushirikiana na Vitengo Maalum vya Ufuatiliaji katika Wizara. Taarifa za Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa zitachambuliwa kwa kuzingatia viashiria vikuu vya utekelezaji vilivyoainishwa wakati wa uchambuzi wa kina wa kimaabara.

Ratiba ya uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2016/17 ipo katika **Kiambatisho II.**

SURA YA SITA

VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO

6.1 Utangulizi

Vihatarishi mbalimbali vinaweza kujitokeza katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, kuna umuhimu wa kukabiliana na vihatarishi vya Mpango ili kuzuia athari zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa Mpango.

6.2 Vihatarishi katika kutekeleza Mpango

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17 unaweza kuathiriwa na vihatarishi vifuatavyo:-

(a) **Mikopo na Misaada:** Mikopo na misaada kutoka kwa wadau wa maendeleo ni sehemu muhimu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kumekuwa na changamoto katika upatikanaji wa mikopo kwa wakati na riba kubwa hivyo kuathiri uwezo wa nchi kukopa. Kwa upande wa misaada kumekuwepo na masharti magumu na utayari wa washirika wa maendeleo kutoa fedha kwa wakati. Hali hii huathiri kwa kiasi kikubwa kasi ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo;

(b) **Riba za Mikopo:** Kasi ndogo ya kupungua kwa viwango vya riba katika taasisi za fedha za hapa nchini na hivyo kuathiri uwezo wa wawekezaji kukopa. Aidha, viwango vikubwa vya riba vinapunguza thamani ya mitaji ya uwekezaji kwa sekta ya umma na binafsi;

(c) **Mfumuko wa Bei:** Kuongezeka kwa bei za chakula, nishati, vifaa vya ujenzi na vipuri katika soko la ndani na nje kunaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kuongeza gharama za miradi;

(d) **Viwango vya Ubadilishaji Fedha:** Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya fedha za kigeni hususan dola ya Kimarekani imeendelea kushuka. Hali hiyo imetokana na kuimarika kwa uchumi wa Marekani pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya dola za Kimarekani na hivyo kusababisha gharama za uagizaji bidhaa na huduma za miradi kuwa kubwa;

(e) **Mabadiliko ya Tabianchi na Uharibifu wa Mazingira:** Uharibifu wa mazingira na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kunaathiri uendelevu wa rasilimali asili na ikolojia. Hali hii itasababisha kupungua kwa uzalishaji katika sekta za uzalishaji

hususan kilimo, mifugo, uvuvi na utalii; Vile vile, mabadiliko ya hali ya hewa yasiyotabirika kama mvua nyingi au ukame huathiri shughuli nyingi katika utekelezaji wa miradi;

(f) **Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo:** Mahitaji ya nguvu kazi yenye ujuzi, teknolojia, ucheleweshwaji katika ununuzi wa umma, utoaji hafifu wa fedha za maendeleo na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji vinaweza kuathiri utekelezaji wa Mpango;

(g) **Ukuaji wa Miji:** Uanzishwaji wa viwanda utaongeza kasi ya ukuaji wa miji ambao utaathiri utoaji wa huduma za kijamii, usalama na milipuko ya magonjwa, hivyo inaweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na

(h) **Mpango Kutokubalika kwa baadhi ya Makundi katika Jamii:** Mchakato wa kuendeleza sekta ya viwanda unaweza kukabiliwa na pingamizi kutoka kwa wazalishaji walio sokoni au waagizaji bidhaa na makundi mengine yenye maslahi kutokana na hofu ya kupoteza soko la bidhaa zao. Hali hii inaweza kuathiri uzalishaji na hatimaye ukuaji wa uchumi kwa ujumla.

6.3 Mikakati ya Kukabiliana na Vihatarishi

Serikali kwa kushirikiana na wadau itakabiliana na vihatarishi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuongeza kasi ya upatikanaji wa mikopo na misaada yenye gharama nafuu ikiwemo riba. Serikali kuendelea na jitihada za kupunguza utegemezi kwa kuwianisha mapato na matumizi, kuongeza mapato ya ndani na kuharakisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi;

(b) Kuweka mazingira wezeshi ya biashara hususan katika sekta ya fedha ili kuongeza ushindani miongoni mwa taasisi za fedha na kuwezesha kushuka kwa viwango vya riba. Aidha, Serikali itaongeza makusanyo ya mapato ya ndani ili kupunguza mikopo ya ndani kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi na kutoa fursa kwa sekta binafsi kukopa zaidi kwa ajili ya uwekezaji;

(c) Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na bidhaa za viwandani kwa ajili ya soko la ndani na nje. Aidha, Serikali itaimarisha miundombinu ya nishati na usafirishaji pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa vipuri na vifaa vya ujenzi;

(d) Kuendelea kudhibiti miamala ya fedha za kigeni na kuhamasisha sekta binafsi kuzalisha kwa wingi bidhaa na huduma pamoja na kuongeza thamani ya bidhaa kwa soko la nje ili kuongeza upatikanaji wa fedha

za kigeni;

(e) Kushirikisha wananchi na wadau katika hatua mbalimbali za utunzaji wa mazingira na kujenga uwezo wa kitaasisi katika kuimarisha mifumo itakayosaidia miundombinu kuhimili mabadiliko ya tabia nchi;

(f) Kuhakikisha upatikanaji na uendelezwaji wa nguvu kazi kwa kutekeleza mikakati na programu mbalimbali za uendelezaji rasilimali watu kama ilivyoainishwa kwenye Mpango. Pamoja na hayo Serikali itawekeza zaidi katika miundombinu wezeshi kwa maendeleo ya viwanda ili kupunguza gharama na kuongeza uzalishaji nchini;

(g) Kuhakikisha uwepo wa mipango miji inayoendana na kasi ya ukuaji wa miji ili kurahisisha utoaji wa huduma za kijamii; na

(h) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari, taasisi za elimu, vyama vya wazalishaji, wasambazaji na walaji, itaendelea kutoa elimu ya Mpango na namna bora ya utekelezaji ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika miradi ya Maendeleo. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na mahusiano mazuri na Washirika wa Maendeleo katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

Kiambatisho I

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 2014/15

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
Reli	Kubadilisha km 197 za njia ya reli ya kati kwa kuweka reli ya kiwango cha ratili 80 kwa yadi	• Ununuzi wa mataruma mapya na utandikaji wa reli na mataruma ya uzito wa ratili 80/yadi kati ya Igalula- Tabora - Lulanguru (km 61); • Utandikaji wa reli na mataruma mapya ya uzito wa ratili 80/yadi kati ya Dar es Salaam - Munisagara; na • Ukarabati wa mgodi wa kuzalisha kokoto wa Tura.	• Kukamilisha makabrasha ya zabuni kwa ajili ya wakandarasi wa kutandika reli kati ya Igalula na Tabora (km 37) na kati ya Dar es Salaam na Munisagara (km 52). • Kukarabati mgodi wa kokoto wa Tura - Tabora na mitambo yake ambayo itawezesha uzalishaji wa kokoto kwa ajili ya matengenezo ya njia za reli.
	Ukarabati wa Reli (Kaliua - Mpanda)	• Upembuzi yakinifu wa kipande cha Mpanda - Karema; na • Ukarabati wa tuta la reli kati ya Kaliua - Mpanda.	• Kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa njia ya reli kutoka Kaliua - Mpanda na Mpanda – Karema kwa kiwango cha kimataifa cha standard gauge; na • Kutandika reli za uzito wa ratili 56.12 kwa yadi na kuondoa reli nyepesi na zilizochoka za uzito wa ratili 45 kwa yadi kwa umbali wa km 9 kati ya stesheni za Lumbe, Mto Ugalla na Katumba.
	Ukarabati wa njia kuu ya Reli	• Ukarabati na uimarishaji wa njia ya reli, madaraja na mfumo wa maji kati ya Kilosa na Gulwe; • Tathmini na usanifu wa madaraja ili kuongeza kiwango kufikia uwezo wa	• Kukamilika ujenzi wa daraja katika ya stesheni ya Kitinku – Bahi na madaraja mawili kati ya Kilosa – Gulwe; • Kuanza ujenzi wa madaraja 16 kati ya 25 yaliyopo kati ya Dar es Salaam na Tabora; • Kuendelea na upembuzi yakinifu wa kutafuta suluhisho la

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		tani 25 kwa ekseli; • Usanifu na ujenzi wa madaraja 16 kati ya 25 yenye hali mbaya yaliyopo kati ya Dar es Salaam na Tabora; • Utafiti wa ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la mafuriko yanayoharibu miundombinu ya reli kati ya Kilosa na Gulwe; na • Kuboresha mfumo wa mawasiliano kati ya Dar es Salaam - Dodoma, Tabora - Kigoma na Tabora - Mwanza; kufufua mfumo wa ufuatiliaji wa mizigo; na • Kujenga mabwawa mawili eneo la Kimagai kati ya Godegode na Gulwe (km 351) na Msagali (km 384) kwa ajili ya kuzuia mafuriko.	kudumu katika eneo la Kilosa – Gulwe; na • Kukamilika uundaji wa mfumo wa kufuatilia mizigo kwa majaribio kati ya Dar es Salaam na Morogoro.
	Mradi wa Reli ya Kati ya Isaka – Mwanza	• Kukamilisha usanifu wa kina wa njia ya reli kati ya Isaka – Mwanza; na • Kulipa fidia kwa wakazi wa Buhongwa (hekta 148) ili kupisha mradi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya kupangia na kugeuzia mabehewa.	• Kukamilika kwa usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha kiwango cha *Standard gauge* reli ya Isaka - Mwanza; na • Kuendelea kwa uthamini katika sehemu ya Buhongwa – Mwanza kwa ajili ya kujenga eneo la kupanga na kugeuzia mabehewa.
	Mradi wa Reli Mtwara – Mbamba Bay na Mchuchuma - Liganga	• Kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia ya reli kati ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa	• Kuendelea na upembuzi yakinifu.

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		kiwango cha standard gauge.	
	Reli ya Tanga (Mwambani) – Arusha – Musoma	• Kukamilisha usanifu wa kina kwa kipande cha Tanga - Arusha na mchepuko kati ya Ruvu Junction na Mruazi Junction; na • Kukamilisha upembuzi yakinifu kwa kipande cha Arusha - Musoma na michepuko ya kwenda Minjingu na Engaruka.	• Kuendelea na usanifu wa kina wa kipande cha reli ya Tanga – Arusha na Arusha – Musoma.
	Ujenzi na Uboreshaji wa Reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali/Keza – Msongati	• Kutafuta mwekezaji kwa ajili ya uboreshaji wa reli ya Dar es Salaam - Isaka – Kigali na kuandaa andiko la mradi na nyaraka za zabuni.	• Kuendelea na uandaaji wa andiko la mradi na nyaraka za zabuni kwa mfumo wa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma (PPP).
	Uboreshaji wa Njia ya Reli ya TAZARA	• Kukarabati karakana ya Dar es Salaam, mtambo wa kuzalisha kokoto uliopo Kongolo (Mbeya) na kuboresha vituo vya kupandia abiria Dar es Salaam.	• Kukarabati mtambo wa kuzalisha kokoto wa Kongolo – Mbeya; na • Kubadilishwa mataruma 8,900 ya zege na 3422 ya mbao.
	Usafiri wa Treni ya Abiria - Dar es Salaam	• Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli katika jiji la Dar es Salaam katika maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Bagamoyo; na • Ujenzi wa mchepuko wa njia ya reli kutoka “Ilala block post” hadi Stesheni.	• Kusainiwa mkataba kwa ajili upembuzi yakinifu wa njia mpya za reli itakayounganisha miji ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/ Kibaha na Bunju/ Bagamoyo.

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
Bandari **A. Bahari Kuu**	Bandari ya Dar es Salaam	• Ujenzi wa gati Na. 1 – 7 ikijumuisha gati Na. 4 la magari na gati Na. 5-7 la makasha • Ujenzi wa gati Na. 13 - 14 na • Ununuzi wa chelezo katika bandari ya Dar es Salaam	• Kukamilisha taarifa ya uchambuzi wa zabuni ya huduma ya kusimamia na kuimarisha gati Na. 1 – 7 ikijumuisha ujenzi wa gati Na. 4 la magari na upembuzi yakinifu wa kubadili gati Na. 5 - 7 kuwa gati la makasha (container terminal); • Kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati Na. 13 na 14; na • Kutangazwa kwa zabuni ya awali (Expression of Interest) kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Chelezo.
	Bandari ya Mtwara	• Kuboresha miundombinu, kununua vifaa vya kuhudumia shehena na kuanza maandalizi ya ujenzi wa magati mapya 4.	• Kuanza maandalizi ya kutekeleza mradi awamu ya kwanza ya ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita mia tatu (300).
	Bandari ya Mbegani - Bagamoyo	• Kulipa fidia katika eneo la mradi.	• Kusainiwa kwa makubaliano (MoU) na kuendelea na majadiliano baina ya Serikali ya Tanzania, Kampuni ya China *Merchants Holding International na General State Reserve Funds* ya Oman; na • Kukamilika kwa kazi ya uthamini katika eneo la bandari lenye ukubwa wa ekari 887 na kuendelea na ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha mradi.
	Bandari ya Mwambani, Tanga	• Kuanza maandalizi ya ujenzi wa bandari mpya ya Mwambani.	• Kupitia upya taarifa ya upembuzi yakinifu ili kuiboresha kwa kujumuisha matarajio ya kuongeza shehena ya kutosha kuvutia wawekezaji.
B. Maziwa Makuu	Bandari ya Kigoma	• Kukamilisha ujenzi wa magati ya Karema, Lagosa, Sibwesa na Kagunga; • Kuanza ujenzi wa bandari kavu ya Katosho na ujenzi wa jengo la abiria	• Kumtafuta Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuendeleza bandari ya Karema; • Kuendelea na majadiliano na Mkandarasi M/S Kashere Enterprises kwa ajili ya ujenzi wa gati la Lagosa;

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		katika bandari ya Kigoma.	• Kuendelea kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bandari ya kigoma; • Kukamilika kwa tathmini ya mazingira kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria katika bandari ya Kigoma; na • Kuanza ujenzi wa gati la Sibwesa na Kagunga
C.Bandari Kavu	Bandari Kavu ya Kisarawe	• Kukamilisha upembuzi yakinifu awamu ya pili, • Kuanza usanifu wa kina; • Kuandaa michoro; na • Uthamini wa fidia.	• Kupewa mkataba wa kufanya upembuzi yakinifu kwa Kampuni ya Royal Haskoning ya Uholanzi ambapo mradi huu unatarajiwa kutekelezwa kwa kushirikisha Sekta Binafsi (Public-Private Partnership-PPP).
Barabara	Barabara Kuu	• Ujenzi wa kilometa 560.3 na ukarabati wa kilomita 131.5 za barabara kuu kwa kiwango cha lami.	• Kukamilika kwa ujenzi wa kilometa 542.6 za barabara kuu kwa kiwango cha lami; na • Kukarabati kilometa 102.09 za barabara kuu kwa kiwango cha lami.
	Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396):	• Kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.	• Kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.
	Barabara ya Itoni – Mkiu – Ludewa – Manda (km 211):	• Kukamilisha upembuzi yakinifu na kuanza ujenzi wa km 50 kwa kiwango cha lami.	• Kukamilika Upembuzi yakinifu; na • Kukamilika ukarabati kwa kiwango cha changarawe na kufanikisha usafirishaji wa vifaa vya mwekezaji hadi eneo la miradi, Mchuchuma na Liganga.
	Barabara ya Sumbawanga – Mpanda - Uvinza –	• Kukamilisha km 100 kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Kidahwe – Kasulu – Nyakanazi (km 310);	• Barabara ya Sumbawanga – Kanazi: Ujenzi wa tuta la barabara km 50.71, tabaka la chini la msingi km 43.49, tabaka la juu la msingi km 43.48, na tabaka la lami km 43.47. Ujenzi wa

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
	Kanyani - Kasulu - Nyakanazi (km 770.9) na Kidahwe – Kanyani – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 310):	• Kujenga kwa awamu barabara ya Sumbawanga – Mpanda - Uvinza – Kanyani - Kasulu – Kibondo – Nyakanazi kwa kuanza na sehemu ya Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi - Kibaoni (km 76.6), Kizi – Sitalike – Mpanda (km 36.9) na Mpanda – Mishamo (km 100).	barabara umefikia asilimia 68.60; • Barabara ya Kanazi – Kizi – Kibaoni: Ujenzi wa tuta la barabara km 28.56, tabaka la chini la msingi km 16.52, tabaka la juu la msingi km 16.37 na tabaka la lami km 16.37 Ujenzi wa barabara umefikia asilimia 43.55; • Barabara ya Sitalike – Mpanda: Ujenzi wa tuta la barabara km 33.7, tabaka la kwanza la msingi km 21.2, tabaka la juu km 120.8 na tabaka la lami km 16.37. Ujenzi wa barabara umefikia asilimia 76; • Barabara ya Kidahwe – Kasulu: Ujenzi km 50 umefikia asilimia 10; na • Barabara ya Nyakanazi – Kibondo: Ujenzi km 50 umefikia asilimia 11.95.
	Barabara ya Mbeya – Makongorosi – Rungwa – Itigi - Mkiwa (km 528):	• Kuendelea kujenga barabara kwa kiwango cha lami katika sehemu tatu za utekelezaji ambazo ni: Mbeya - Lwanjilo (km 36), Lwanjilo - Chunya (km 36), na kipande cha Chunya – Makongorosi (km 43); na kukarabati barabara ya Makongorosi – Rungwa - Itigi - Mkiwa (km 413) kwa kiwango cha changarawe.	• Barabara ya Mbeya – Lwanjilo: Kukamilika ujenzi wa tuta la barabara km 36, tabaka la chini km 24, tabaka la juu km 23 na ujenzi wa tabaka la lami km 31.2 ambapo ujenzi umefikia asilimia 86; • Barabara ya Lwanjilo – Chunya: Ujenzi umekamilika na barabara ipo katika kipindi cha uangalizi.
	Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 264.35):	• Kuendelea kujenga barabara kwa kiwango cha lami katika sehemu tatu za utekelezaji ambazo ni: Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35), Chaya - Nyahua	• Manyoni – Itigi – Chaya: Ujenzi wa tuta la barabara km 89.30, tabaka la chini la msingi km 89.30, tabaka la juu la msingi km 89.30 na tabaka la lami km 89.30 barabara ya Manyoni – Itigi – Chaya. Ujenzi umefikia asilimia 98.25;

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		(km 90), na Nyahua – Tabora (km 85).	• Tabora – Nyahua: Kujenga tuta la barabara km 75.65, tabaka la msingi km 73.98, tabaka la juu km 68.85 na tabaka la lami km 66.42. Ujenzi umefikia asilimia 86.7; • Chaya – Nyahua: upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea.
	Barabara ya Tunduma – Sumbawanga (km 223.2):	• Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Laela – Sumbawanga na kuanza ujenzi wa sehemu ya Tunduma mjini (km 1.6).	• Kukamilika kwa ujenzi wa barabara Februari 2015.
	Barabara ya Dodoma – Babati (km 251.4):	• Ujenzi wa barabara katika sehemu tatu za utekelezaji ambazo ni Dodoma – Mayamaya, Mayamaya – Mela, Mela - Bonga na kulipa sehemu ya madai ya mkandarasi aliyekamilisha ujenzi wa barabara ya Bonga – Babati.	• Barabara ya Dodoma – Mayamaya: Ujenzi wa tuta la barabara km 37.1, tabaka la la msingi km 35, tabaka la juu km 35 na tabaka la lami km 35 na makalvati 200 ambapo ujenzi umefikia asilimia 80; • Barabara ya Mayamaya – Mela: ujenzi wa tuta la barabara km 35.53, tabaka la msingi km 2.27, Ujenzi umefikia asilimia 24.02 na • Barabara ya Mela – Bonga: ujenzi wa tuta la barabara km 30.45. Ujenzi umefikia asilimia 24.21.
	Barabara ya Iringa – Dodoma (km 259.8):	• Ujenzi wa barabara katika sehemu tatu kwa kiwango cha lami za Iringa – Migori (km 95.1), Migori – Fufu (km 93.8), na Fufu – Dodoma (km 70.9).	• Kukamilika kwa ujenzi wa barabara Juni 2015.
	Barabara ya Masasi - Songea – Mbamba Bay (km 1,154.7):	• Ujenzi wa barabara katika sehemu za Mangaka – Nakapanya – Tunduru (km 137), Mangaka – Mtambaswala (km 65.5), Tunduru – Matemanga (km 58.7), Matemanga – Kilimasera (km	• Ujenzi wa barabara ya Mangaka – Nakapanya umefikia asilimia 14.8, kwa barabara ya Nakapanya – Tunduru asilimia 13 na barabara ya Mangaka – Mtambaswala asilimia 18.4; • Barabara ya Kilimasera – Namtumbo: ujenzi wa tuta la barabara km 28, tabaka la chini km 23, tabaka la juu km 11.

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		68.2), na Kilimasera – Namtumbo (km 60.7) na kuanza ujenzi wa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66).	Ujenzi umefikia asilimia 30.8; na • Barabara za Tunduru – Matemanga na Matemanga – Kilimasera ipo katika hatua ya kukusanya vifaa kwa ajili ya kuanza ujenzi; na • Usanifu wa kina umekamilika kwa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay na kwa upande wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi, upembuzi yakinifu unaendelea na unatarajiwa kukamilika Novemba 2015
	Barabara ya Bagamoyo (Makurunge) - Sadani – Tanga (km 178):	• Kukamilisha usanifu wa kina na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.	• Kukamilika kwa usanifu wa kina wa barabara.
	Barabara ya Ndundu - Somanga (km 60):	• Kukamilisha ujenzi wa barabara	• Ujenzi wa barabara umekamilika Februari 2015 na ipo katika kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja.
	Barabara ya Mwigumbwi – Maswa – Bariadi - Lamadi (km 171.8):	• Ujenzi wa kipande cha Bariadi - Lamadi (km 71.8) kwa kiwango cha lami.	• Ujenzi wa tuta la barabara km 77, tabaka la chini la msingi km 66.5, tabaka la juu km 66 na tabaka la lami km 65. Barabara imekamilika kwa asilimia 93.
	Barabara ya Arusha – Namanga (km 105):	• Kukamilisha ujenzi wa barabara kwa ujenzi wa Kituo cha Utoaji Huduma kwa Pamoja Mpakani	• Ujenzi wa Kituo cha Utoaji Huduma kwa Pamoja Mpakani umekamilika Januari 2015.
	Barabara ya Nyanguge – Musoma (km 183) na michepuko ya Usagara – Kisesa (km	• Ujenzi kwa kiwango cha lami katika sehemu nne za Simiyu/Mara Border – Musoma, Kisesa – Usagara, Kisorya – Bunda na Nyamuswa – Bunda	• Kukamilika kwa barabara ya Simiyu/Mara Boarder – Musoma sehemu ya Simiyu - Musoma km 85.5; • Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kisesa – Usagara ambapo ujenzi wa tuta la barabara umefikia km 13.48 na tabaka la chini km 2.6; na

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
	17) na Bulamba – Kisorya (km 51):		• Kuanza ujenzi wa sehemu ya Nyamuswa – Bunda.
	Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242), Lusahunga – Rusumo (km 92) na Nyakasanza – Kobero (km 60):	• kukamilisha malipo ya mkandarasi wa barabara ya Isaka - Ushirombo na kuendelea na ukarabati sehemu ya Ushirombo – Lusahunga.	• Barabara ya Ushirombo – Lusahunga: Kujenga tuta, tabaka la chini la msingi na la juu pamoja na uwekaji wa tabaka la lami km 54. Ujenzi wa barabara hii umefikia asilimia 51. • Barabara za Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero usanifu wa kina umekamilika.
	Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112):	• Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.	• Kusafisha njia, kujenga tuta la barabara km 65, tabaka la chini la msingi km 59, tabaka la juu km 56 na tabaka la lami km 56 ambapo ujenzi wa barabara hii umefikia asilimia 52.2.
	Barabara ya Arusha – Moshi – Holili na Arusha Bypass (km 140):	• Kuanza kazi ya kupanua barabara kuwa njia nne kwa kiwango cha lami sehemu ya Sakina – Tengeru (km 14.1) na barabara ya mchepuko (Arusha Bypass km 42.41). Ni lengo au utekelezaji	• Kumpata Mkandarasi na kusaini mkataba wa ujenzi.
	Barabara za Mikoa	• Ujenzi wa barabara km 94 kwa kiwango cha lami, • Ukarabati wa barabara km 1,350 kwa kiwango cha changarawe, na • Ujenzi wa madaraja 14..	• Kukamilika kwa ujenzi wa km 51.7 sawa na asilimia 52.3 ya lengo la mwaka; na • Kukarabati km 343.8 kwa kiwango cha changarawe sawa na asilimia 21.5 ya lengo
	Barabara za Kupunguza Msongamano Mijini (km 109.35)	• Ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam zenye urefu wa km 109.35	• Kigogo Roundabout - Bonde la Msimbazi - Twiga/Msimbazi Junction (km 2.7): ujenzi wa tuta la barabara km 2.7, tabaka la msingi na tabaka la juu na la lami km 2.3 ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 86;

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
			• Tabata Dampo – Kigogo (km 1.65) na Ubungo Maziwa - External (km 2.25): Kazi za ujenzi kwa sehemu ya Tabata Dampo – Kigogo (km 1.65) zimefikia asilimia 72; • Kimara Kilungule – Maji chumvi - External Mandela Road (km 9): awamu ya kwanza ya kutoka makutano ya barabara ya External na Mandela hadi Maji Chumvi (km 3), ujenzi umefikia asilimia 75; • Mbezi (Morogoro Road) – Malambamawili - Kinyerezi - Banana (km 14): Awamu ya kwanza ya kutoka Kinyerezi hadi Kifuru (km 4) ujenzi umefikia asilimia 67; • Tegeta Kibaoni - Wazo – Goba - Mbezi Mwisho (km 20): ujenzi umefikia asilimia 56 kwa kipande cha barabara ya Goba – Mbezi Mwisho yenye km 7; • Tangi Bovu - Goba (km 9): ujenzi umefikia asilimia 54; • Kimara Baruti – Msewe - Changanyikeni (km 2.6): ujenzi umefikia asilimia 39; • Kibamba – Kisopwa (km 12): kipande cha Kibamba – Mloganzila (km 4) ujenzi umekamilika Februari, 2015 upo katika kipindi cha uangalizi hadi Februari, 2016; • Ujenzi wa mradi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka na vituo vyake upo katika hatua za mwisho za utekelezaji.
	Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyover)	• Ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya TAZARA, • kuboresha makutano ya Chang'ombe, Ubungo, Uhasibu, KAMATA,	• Zabuni kwa ajili ya kupata mkandarasi wa kujenga barabara za juu eneo la TAZARA imetangazwa; • Tathmini mali zitakazofidiwa eneo la mradi wa barabara ya juu katika makutano ya Ubungo imekamilika na Mhandisi Mshauri

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco na • Upembuzi yakinifu wa upanuzi wa barabara ya Nyerere kuanzia TAZARA – JNIA (km 6.0) kuwa njia 6.	anafanya mapitio ya usanifu na kuandaa nyaraka za zabuni; na • Mchakato wa kuanza usanifu wa kina kwa barabara ya Nyerere kuanzia eneo la TAZARA – JNIA unaendelea
	Mradi wa Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (km 200)	• Kumpata Mtaalam Mshauri (Transaction Advisor) na • Kukamilisha upembuzi yakinifu kwa km 100 za awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Chalinze.	• Hatua iliyofikiwa ni kupatikana kwa Mtaalam Mshauri na anaendelea na kazi ya usanifu wa kina.
	Madaraja	• Ujenzi wa madaraja 6 ya Mbutu, Kigamboni, Kavuu, Kilombero, Lukuledi II na Sibiti, • Kukarabati daraja la Kirumi, • Usanifu wa daraja la Ruhuhu na • Upembuzi yakinifu madaraja 2 ya Selander na Momba .	• Kuendelea na ujenzi wa madaraja ambapo daraja la Mbutu asilimia 99, Kigamboni limefikia asilimia 92, Kavuu asilimia 40, Kilombero asilimia 27.58, Lukuledi II asilimia 90, na Sibiti asilimia 22; • Kukamilika kwa taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kupitia usanifu wa nyaya zinazoshikilia daraja *(design review of cable strays)* na kusimamia kazi ya ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara); • Kuendelea na usanifu wa daraja la Ruhuhu (Ruvuma); na • Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa madaraja ya Selander na Momba.
	Vivuko na Maegesho ya Vivuko	• Kutafuta Mkandarasi wa ujenzi wa kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni; • Ununuzi wa kivuko kipya kati ya Dar es Salaam – Bagamoyo; na	• Kukamilika kwa ununuzi wa kivuko kipya cha Dar es Salaam na Bagamoyo; na • Kukamilika kwa uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya kupata mkandarasi wa kukarabati kivuko cha MV Magogoni.

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		• Ukarabati wa vivuko vya MV Mwanza (Mwanza), MV Pangani II (Pangani – Tanga), MV Kiu (Kilombero) na MV Magogoni (Dar es Salaam).	
Nishati	Bomba la Gesi Asilia Mtwara & Lindi - Dar es Salaam (km 542)	• Kukamilisha ujenzi wa bomba la gesi; na • Kukamilisha ujenzi wa mitambo ya kuchakata gesi asilia na majaribio ya awali ya kuwasha mitambo.	• Kukamilika kwa ujenzi wa bomba la gesi na mitambo ya kusafisha gesi katika maeneo ya Madimba na Songosongo; • Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 32 zenye uwezo wa kuhudumia wafanyakazi 172 katika maeneo ya Madimba na Songosongo;
	Mtambo wa Kufua Umeme Kinyerezi I (MW 150)	• Kukamilisha usimikaji wa mitambo ya kufua umeme; • Kujenga kituo cha kupoza umeme (kV 220/400); • Kujenga njia ya kusafirisha umeme wa kV 220 kutoka Kinyerezi hadi Kimara ambao utaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa; na • Kujenga njia ya msongo wa kV 132 kutoka Kinyerezi hadi Gongo la Mboto - Dar es salaam.	• Kukamilika kwa ujenzi wa mradi na njia za usafirishaji wa umeme na kuanza majaribio ya kuzalisha umeme unaoingizwa kwenye gridi ya Taifa.
	Mtambo wa Kufua Umeme Kinyerezi II (MW 240)	• Kupatikana mkopo wa asilimia 85 ya gharama ya mradi kutoka Sumitomo Mitsui Banking Corporation na Japan Bank of International Cooperation (JBIC) na kuagiza mitambo	• Kukamilika kwa majadiliano na kusaini mkataba wa mkopo na kampuni ya JBIC ambapo mkopo ni sawa na asilimia 85 ya gharama za mradi. Hadi Agosti 2015, Serikali imetoa shilingi bilioni 60 sawa na asilimia 9 kati ya 15 inayohitajika. • Mkandarasi, Kampuni ya Somitomo imeanza kazi ya usanifu wa mradi.

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
	Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo kV 220 Makambako – Songea (km 250)	• Kulipa fidia na malipo ya awali ya wakandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi; na • Kujenga vituo 2 vya kupoza umeme (kV 220/33) katika eneo la Madaba na Songea mjini pamoja na njia za kusambaza umeme wa msongo wa kV 33.	• Ulipaji wa fidia shilingi bilioni 6.72 kwa wananchi 1,804 katika Mikoa ya Njombe na Ruvuma. Hata hivyo wananchi 8 hawajalipwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kutokubaliana na kiwango cha fidia; na • Kuendelea na kazi ya usanifu wa njia ya kusambaza umeme.
	Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 Iringa - Shinyanga (km 670)	• Ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme.	• Kujenga nguzo 480 kati ya 594 kwa Lot Na. 1, nguzo 78 kati ya 586 kwa Lot Na. 2 na nguzo 361 kati ya 594 kwa Lot Na. 3. Ujenzi wa mradi huu umefikia asilimia 48.
	Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 *North West Grid* (Mbeya – Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi km 1,148)	• Kuboresha upembuzi yakinifu na usanifu uliopo wa njia ya umeme wa msongo wa kV 220 ili kuwiana na mahitaji ya sasa ya kujenga njia hiyo kwa kiwango cha kV 400; na • Kupima mkuza wa njia ya umeme kutoka Mbeya hadi Sumbawanga (km 340) na kulipa fidia ya mali zitakazoathiriwa na mradi kwenye njia ya Mbeya - Sumbawanga.	• Kuendelea kuboresha upembuzi yakinifu na usanifu wa kubadilisha msongo wa umeme kutoka kV 220 hadi kV 400 unaotekelezwa na kampuni ya SWECO; • Kukamilika kwa upimaji wa kilomita 321 za mkuza wa njia ya umeme kutoka Mbeya hadi Sumbawanga; • Kupatikana kwa mshauri kampuni ya SWECO kwa ajili ya usanifu wa mradi; na • Kupata cheti cha mazingira kutoka Baraza la Taifa la Mazingira.
	Mradi wa msongo wa kV 400 North - East Grid (Dar – Tanga – Arusha km 682)	• Upimaji wa ardhi na kuweka mipaka ya ukomo wa eneo la mradi; • Kulipa fidia eneo ambalo njia ya usafirishaji umeme itapita; na	• Kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya mradi; • Kuendelea na upimaji wa ardhi na kuweka mipaka ya ukomo wa mradi kutoka sehemu ya Kinyerezi (Dar es Salaam) hadi Chalinze (Pwani); na

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		• Kumpata mshauri mwelekezi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji.	• Kukamilika kwa tathmini ya mazingira.
	Miradi ya Umeme Vijijini	• Kutekeleza Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini katika mikoa mbalimbali Tanzania Bara.	• Kuunganishwa kwa wateja wapya 30,173 kupitia miradi ya usambazaji wa umeme vijijini inayotekelezwa na REA katika mikoa 20 ya Tanzania Bara.
	Mradi wa kusambaza umeme katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Shinyanga na Geita *(Mradi wa Electricity V):*	• Kukamilisha ukarabati wa vituo vya kupoza umeme vya Ilala (kV 132/33/11) na Sokoine Drive (kV 33/11) vilivyopo Dar es Salaam na kituo cha Njiro (kV 220/132/33) kilichopo Arusha.	• Ukarabati wa vituo vya Ilala umefikia asilimia 98; • Ujenzi wa msingi katika kituo cha Sokoine umekamilika kwa asilimia 70; • Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa kituo cha Njiro; na • Kazi ya ufungaji mitambo katika kituo cha Ilala imefikia asilimia 14 na Njiro asilimia 25.
Teknolojia ya Habari na Mawasiliano	Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano	• Kuendelea na Ujenzi Awamu ya III sehemu ya kwanza inayohusu kupanua mkongo kwa baadhi ya maeneo ambayo hayakufikiwa katika awamu ya I na ya II; • Kuunganisha Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; • Kuunganisha Tanzania na mikongo ya baharini ya SEACOM na ESSy; • Kuunganisha Tanzania na nchi jirani; • Ujenzi wa jengo la Data Centre katika eneo la Kijitonyama; na • Kuendelea na Ujenzi wa Mikongo ya	• Kukamilika kwa ujezi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano awamu ya I na II km 7,560; • Kuendelea kuunganisha Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; • Kuendelea na ujenzi wa jengo la Data Center katika eneo la Kijitonyama; na • Kukamilika kwa utekelezaji wa ujenzi wa Mikongo ya mijini katika mikoa ya Mwanza (km 36) na Arusha (km 58). Ujenzi wa mikongo unaendelea katika mikoa ya Morogoro (km 18), Dodoma (km42), Kilimanjaro (km 35.08) na Tanga (km 43.28).

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		Mijini katika miji ya Morogoro, Arusha, Mwanza na Dodoma.	
	Maeneo Maalum ya TEHAMA (ICT Park)	• Kulipa fidia na kuanza ujenzi wa kituo mahiri cha TEHAMA katika eneo maalum la uwekezaji EPZ Bagamoyo.	• Kukamilika kwa malipo ya fidia shilingi bilioni 1.7 kwa wananchi 9 na taasisi 2 katika eneo la mradi lenye ekari 438.
Maji	Mradi wa Maji wa Ruvu Chini – Pwani	• Kukamilisha ulazaji wa mabomba kutoka Ruvu Chini hadi kwenye matanki yaliyopo maeneo ya Chuo Kikuu Ardhi.	• Kazi ya ulazaji wa mabomba kutoka eneo la mradi (Bagamoyo) hadi Dar es Salaam imekamilika km 54.43 kati ya km 55.93 za mradi wote sawa na asilimia 97. Mradi unatarajiwa kuongeza uwezo wa uzalishaji maji kutoka mita za ujazo 182,000 hadi 272,000 kwa siku.
	Mradi wa Maji Ruvu Juu – Pwani	• Kuanza ujenzi wa miundombinu ya maji kutoka Ruvu Juu hadi Kimara - Dar es Salaam.	• Kazi ya upanuzi wa chanzo cha maji eneo la Ruvu Darajani na mitambo ya kusafisha maji eneo la Mlandizi unaendelea ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 64; na • Ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara na ujenzi wa tanki la Kibamba umefikia asilimia 43.
	Bwawa la Kidunda – Morogoro	• Kulipa fidia kwa wananchi waliopo katika eneo linalozunguka bwawa na barabara yenye urefu wa km 76 kutoka Ngerengere hadi Kidunda; na • Kuandaa mazingira ya kuvutia wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Kidunda	• Wananchi wamelipwa fidia ya shilingi bilioni 3.005 kupisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 76 kutoka Ngerengere hadi bwawa la Kidunda; • Wananchi wamelipwa fidia ya shilingi bilioni 4.478 kupisha eneo litakapojengwa bwawa; • DAWASA imeingia makubaliano na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ili kuandaa viwanja 1,000 vya kuhamishia wananchi watakaopisha eneo la mradi na barabara; na • Taarifa ya athari za kimazingira na kijamii imekamilika
	Mradi wa Visima	• Utafutaji, uchimbaji wa visima 20 na	• Kukamilika kwa uchimbaji wa visima 6 kati ya 20 ambapo

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
	Virefu vya Kimbiji - Dar es Salaam na Mpera - Pwani	uandaaji wa miundombinu ya kusambaza maji katika eneo la Kimbiji, Kigamboni (Dar es Salaam) na Mpera, Kisarawe (Pwani).	visima 3 vimechimbwa Kimbiji na visima 3 Mpera.
	Mradi wa Maji Same - Mwanga - Korogwe	• Ujenzi wa kingio la maji, matanki ya kuhifadhia maji na kujenga bomba kuu katika mradi wa kupeleka maji katika miji ya Same na Mwanga.	• Mkandarasi kukabidhiwa eneo la mradi kwa ajili ya kuanza kazi.
	Miradi ya Maji Vijijini	• Kutekeleza miradi ya maji ya vijiji kumi na uchimbaji wa mabwawa vijijini.	• Miradi ya maji mipya 975 imejengwa katika vijiji 1,206 vyenye vituo 24,129 katika Halmashauri 148.
	Upanuzi wa Mradi wa Maji Ziwa Victoria – Shinyanga – Kahama	• Kukamilisha usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya majisafi kutoka bomba kuu la Ziwa Victoria kwenda miji ya Tabora, Igunga na Nzega na miji midogo ya Isaka, Kagongwa na Tinde.	• Usanifu wa ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya miradi ya maji kwa miji ya Tabora, Igunga na Nzega umekamilika na vitabu vya zabuni vimeandaliwa; • Taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya usanifu mradi wa kupeleka maji katika miji midogo ya Isaka, Kagongwa na Tinde zinaendelea.
	Miradi ya Maji ya Kitaifa	• Kukarabati miundombinu ya maji katika miradi mikubwa 7 ya Chalinze (Pwani), Handeni TrunkMain (Tanga), Kahama - Shinyanga (Shinyanga), Mugango - Kiabakari (Mara), Makonde (Mtwara), Maswa (Simiyu) na Wanging‟ombe (Njombe) . ili kuongeza ufanisi.	• Serikali imeendelea kuhudumia miradi ya maji ya Kitaifa kwa kukarabati miundombinu ya maji, ununuzi wa pampu, mabomba na kugharamia umeme kwa ajili ya kuendeshea mitambo.
Kilimo	Uwekezaji katika	• Kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji	• Mashamba makubwa 4 yenye hekta 117,800 ya Kitengule,

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
	Kilimo cha Miwa na Mpunga	katika kilimo cha miwa na mpunga katika mashamba 8 kwenye mabonde ya Wami, Ruvu, Rufiji, Kagera, Kilombero na Malagarasi ambayo ni Kitengule (Karagwe), Kasulu (Kasulu), Kumsenga (Kibondo), Kisaki (Morogoro), Mvuha (Morogoro), Mahurunga (Mtwara), Ikongo (Serengeti/ Butiama) na Misegese (Ulanga).	Bagamoyo, Lukulilo na Mkulazi kati ya mashamba 8 yamehakikiwa na kupatiwa hati miliki; • Kupatikana kwa watoa huduma binafsi kwa ajili ya skimu 30 za umwagiliaji katika Wilaya za Mbarali, Kyela na Iringa ambapo uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka tani 4.1 hadi 5.0 kwa hekta; • Mipaka ya mashamba 3 ya Muhoro, Mahurunga na Tawi imehakikiwa; • mashamba makubwa 9 ya uwekezaji ya Mpanga-Ngalamila, Lukulilo, Bagamoyo, Kasulu, Muhoro, Tawi, Kitengule, Mkulazi na Pangani yamepimwa; • Mashamba ya Kasulu, na Mahuranga yako katika mchakato wa kuhaulishwa kutoka ardhi ya kijiji kwenda ardhi ya umma ambapo mashamba ya Mvuha na Kisaki yako katika ngazi za upimaji; • Hekta 43,200 za mashamba ya wakulima wadogo zimehakikiwa k na jumla ya Hati za Hakimiliki za Kimila 1,513 zimeandaliwa kwa wakulima wanaozunguka shamba la Lukulilo na Ngalimila; • Vijiji 64 vinavyozunguka mashamba makubwa 13 ya uwekezaji vimeanza kutekeleza mpango-kina wa matumizi bora ya ardhi.
	Skimu 78 za umwagiliaji Mpunga	• Kuendeleza skimu 39 zenye jumla ya hekta 21,738 katika Wilaya za Sumbawanga, Mpanda, Mlele, Mbarali, Iringa, Kilombero, Mvomero, Kilosa na Morogoro Vijijini kwa kufanya mapitio	• Kuendelea kwa ujenzi wa skimu 19 zenye hekta 9,709 ambapo wananchi 69,681 watanufaika na skimu za Msolwa Ujamaa, Signali na Mkula (Kilombero), Rudewa na Mvumi (Wilaya ya Kilosa), Sakalilo (Wilaya ya Sumbawanga), Ipatagwa na Kapyo (Mbalali), Chang'ombe, Motombaya, Kongolo Mswiswi,

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		ya usanifu na kukarabati/kujenga skimu hizo; • Ujenzi wa barabara za kufika kwenye skimu; kupata mtoa huduma binafsi; na • Ujenzi na ukarabati wa maghala 5 ya kuhifadhia mpunga kutoka katika skimu 39.	Mwendamtitu na Gwiri (Wilaya ya Mbarali), Idodi, Mapogoro na Cherehani Mkoga (Wilaya ya Iringa) na Ugala, Karema, Mwamkulu (Wilaya ya Mpanda); na • Ukarabati na ujenzi wa miundombinu katika skimu hizo 19 za umwagiliaji upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. • Kukamilika kwa usanifu na kupatikana kwa wakandarasi wa ujenzi wa Maghala 8 katika skimu 8 za umwagiliaji za Ngana na Makwale (Kyela), Magozi na Tungamalenga (Iringa Vijijini) na Mbuyuni, Kimani, Ipatagwa, Kongolo Mswiswi na Motombaya (Mbarali).
	Kilimo cha Mahindi	• Kujenga maghala ya masoko 275 (*Collective Warehouse Based Marketing Schemes* – COWABAMA) kwa ajili ya mazao ya mahindi katika ukanda wa SAGCOT ili kuhifadhi mahindi kwa ubora na kuongeza thamani.	• Kukamilisha ujenzi wa maghala mapya 2 katika Wilaya za Mlele na Nsimbo; • Ukarabati wa maghala 36 katika mikoa ya Iringa (12), Njombe (4) na Songea (20) unaendelea. • Kupatikana kwa Mtaalam Mwelekezi wa kujenga mfumo/ kanzidata ya COWABAMA kwa ajili ya kufanikisha uchambuzi wa usambazaji wa taarifa za masoko kwa wadau.
	Uendelezaji wa Skimu za Umwagiliaji	• Kujenga na kukarabati maghala 6 katika skimu za Lekitatu, Uturo, Mombo, Bagamoyo, Mkindo na Mkula; na • Kuendelea na ujenzi wa skimu ya Itete (hekta 1000).	• Ujenzi wa banio na mifereji mikuu ya kulia yenye urefu wa km 2.46 na kushoto km 4.17 na miundombinu ya mashamba katika skimu ya Itete umekamilika.
	Tafiti za Kilimo	• Kuimarisha tafiti za kilimo ili kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora zinazohimili ukame; na	• Tafiti zimewezesha kuidhinishwa na kusambazwa kwa miche bora ya kahawa 1,014,671 na aina mpya 65 za mbegu za mazao;

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		• Kukarabati miundombinu katika vituo vya utafiti vya KATRIN, Ukiliguru na Dakawa.	• Kuendelea na maboresho ya kituo cha Kilimo cha Mpunga cha KATRIN - Kilombero (Morogoro) ambapo ukarabati wa miundombinu umefikia asilimia 74; • Kukamilika kwa ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 35 za mashamba ya utafiti ya vituo vya KATRIN na Ukiriguru; na • Ukarabati wa miundombinu ya umeme katika kituo cha utafiti cha Dakawa umefikia asilimia 50.
	Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhi Chakula	• Ujenzi wa ghala la Mbozi kanda ya Makambako lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 na kupata mkandarasi wa kujenga maghala 2 katika kanda ya Songea yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 kila moja.	• Kukamilika kwa ujenzi wa ghala 1 kati ya maghala 2 katika halmashauri ya Songea na • ujenzi wa ghala katika halmashauri ya Mbozi umefikia asilimia 40.
Mifugo	Miundombinu ya Maji na Malisho	• Ujenzi wa malambo ya maji na majosho katika wilaya za Chemba, Handeni, Kiteto, Kilwa, Chunya, Kilindi, Ngorongoro na uchimbaji wa kisima kirefu cha maji kwa matumizi ya mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Same; • Kutenga maeneo kwa ajili ya malisho katika wilaya za Busega, Kiteto, Kilosa, Ngorongoro, Mvomero, Kilindi, Igunga, Iramba na Lindi; na • Kuimarisha mashamba ya malisho ya	• Kuanishwa kwa maeneo yatakayochimbwa malambo kwa ajili ya kunywesha mifugo katika maeneo ya Msomera (Handeni), Pangalua (Chemba) na Masisu (Ngorongoro), kuandaa gharama za ujenzi wa malambo hayo na kuendelea na taratibu za kupata wazabuni watakao fanya kazi ya uchimbaji; • Kuanishwa na kutengwa maeneo ya ufugaji yatakayotumika kuanzisha shamba darasa la kufundishia wafugaji kuhusu uzalishaji, uvunaji na uhifadhi wa malisho katika vijiji vya Manali - Busega (ekari 20), Mwanzugi - Igunga (ekari 2.5) na Partimbo - Kiteto (ekari 20).

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		Vikuge, Langwira, Mpwapwa, Kizota, Uyole, PRC Kongwa na Kondoa LRC.	
	Vituo vya Uhamilishaji	• Ujenzi wa kituo cha kuhifadhi mbegu katika kituo cha Taifa cha Sao Hill - Iringa; • Kusimika mtambo mpya wa kuhifadhi mbegu katika kituo cha Taifa cha Uhamilishaji (NAIC-Usa River); • Kuimarisha vituo 6 vya uhamilishaji vya kanda na kuimarisha mashamba 5 ya kuzalisha mitamba ya Kitulo, Sao Hill, Ngerengere, Mabuki na Nangaramo ili kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mitamba kwa wafugaji.	• Kufanikisha kwa uagizwaji wa vifaa vya uhamilishaji ikiwemo mitungi 9 kwa ajili ya Sao Hill na ukarabati wa mashine ya kukamulia maziwa; • Kukarabati ofisi ya shamba la mitamba la Mabuki na bwawa la mifugo la shamba la mitamba Nangaramo; • Kukarabati mashine ya kukamulia maziwa katika shamba la mitamba la Kitulo; • Ununuzi wa mitamba 30 kwa ajili ya shamba la Ngerengere, 45 kwa shamba la Mabuki na mbegu bora za malisho; na • Kupatiwa hati miliki kwa shamba la mitamba la Nangaramo lenye hekta 56,337.
	Ujenzi wa Minada na Masoko	• Kuanza ujenzi wa minada 2 ya upili ya Longido na Kirumi; na • Kukarabati minada 6 ya upili ya Pugu, Igunga, Weruweru, Meserani, Kizota na Sekenke ili kuwezesha ukusanyaji wa maduhuli na kuzuia upotevu wa mapato	• Kukamilika kwa barabara ya kuzunguka mnada wa upili wa Kizota (Dodoma), kukarabati nyumba za watumishi na kusimika mzani; na • Kukamilika kwa ukarabati wa minada ya Pugu (Ilala), Lumecha (Songea), Kirumi (Butiama) na Nyamatala (Misungwi).
	Upatikanaji wa Pembejeo za Mifugo	• Kutoa ruzuku kwa ajili ya ununuzi wa chanjo na dawa za kuogesha mifugo.	• Kununuliwa kwa lita 119,349 za dawa za kuogesha mifugo kupitia mpango wa ruzuku ya asilimia 40 na kusambazwa katika mikoa 21; na • Ununuzi wa dozi 700,000 za chanjo ya kudhibiti ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo na kusambazwa kupitia vituo vya kanda katika Mikoa ya Arusha (350,000), Mara (100,000),

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
			Pwani (110,000) na Dodoma (140,000).
	Vituo vya Mafunzo na Tafiti za mifugo	• Kujenga na kukarabati Kampasi za Mpwapwa, Madaba, Morogoro, Buhuri, Tengeru na Temeke, vituo vya Mabuki na Kikululai; • Kuendeleza na kuimarisha tafiti za mifugo kwa kukamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa katika kituo cha Chanjo Kibaha; na • Ujenzi na ukarabati wa miundombinu muhimu ya mifugo katika vituo vya utafiti vya Mpwapwa, Mabuki, Naliendele, Kongwa, Tanga, Uyole na West Kilimanjaro.	• Kukamilika kwa ujenzi na kununuliwa vifaa kwa kituo cha chanjo cha Kibaha; na • Kuendelea na ukarabati wa majengo ya Kampasi na kuimarisha vituo vya tafiti za mifugo.
Uvuvi	Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi	• Kukamilisha upembuzi yakinifu na kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi.	• Kukamilika kwa hadidu za rejea kwa ajili ya upembuzi yakinifu utakaowezesha kuanisha eneo kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi.
	Vituo vya Mafunzo na Tafiti za Uvuvi	• Kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) ili kuongeza udahili wa wanafunzi katika kampasi za Mbegani na Nyegezi na vituo vya Gabimiroi, Kigoma na Mwanza South; • Kukarabati maabara na majengo ya vituo vya utafiti; na • Kukarabati Maabara Kuu ya Ukaguzi	• Kuendelea na ukarabati wa majengo ya Kampasi na kuimarisha vituo vya tafiti za uvuvi.

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		wa Mazao ya uvuvi - Dar es Salaam.	
	Huduma ya Uzalishaji wa Samaki	• Ujenzi wa kituo kipya cha kuzalisha vifaranga vya samaki wa maji ya bahari Mtwara, uthamini na kulipa fidia kwa eneo la upanuzi wa kituo; • Kuimarisha vituo vya Mbegani (Bagamoyo) na Machui (Tanga); na • Kuanzisha vituo vipya vya uzalishaji samaki wa maji baridi katika maeneo ya Dareda, Kigoma na Hombolo.	• Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa vituo vya uvuvi vya Kisiju - Mkuranga, Chuno na Msimbati (Mtwara); • Kuimarishwa kwa kituo cha Machui (Tanga) kwa kujenga mabwawa mawili ya kufugia samaki, kumalizika kwa ujenzi wa jengo la kutotolea vifaranga (*hatchery*) na mnara wa kuwekea matangi ya maji; na • Kuanzishwa kwa vituo 2 vya Mwamapuli – Igunga (Tabora) na Nyengedi (Lindi) na kuimarishwa kwa vituo vya Luhira (Ruvuma) na Kingolwira (Morogoro) vya ukuzaji viumbe kwenye maji baridi
Viwanda	Eneo la Bagamoyo SEZ	• Kulipa fidia ya shilingi bilioni 47.5 kwa wananchi 2,180 katika eneo la hekta 5,742.52 (ekari 14,356.3) kutokana na tathmini ya mwaka 2008.	• Ulipaji wa fidia wa shilingi bilioni 7 ambapo jumla ya fidia iliyolipwa hadi sasa ni shilingi bilioni 26.64.
	Kituo cha Biashara na Uwekezaji Kurasini, Dar es Salaam:	• Kukamilisha ulipaji wa fidia na kuandaa eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo.	• Ulipaji fidia wa shilingi bilioni 53 na hivyo kukamilisha fidia ya makadirio ya shilingi bilioni 94.1 kwa tathmini ya mwaka 2013. Hata hivyo kiasi cha shilingi bilioni 3.79 kinahitajika kwa ajili ya fidia kwa baadhi ya maeneo yaliyokuwa na mapungufu na kusafisha eneo la mradi.
	Mradi wa Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma - Liganga	• Kukarabati barabara kutoka eneo la Itoni kuelekea eneo la miradi kwa kiwango cha changarawe; • Kupitia taarifa za usanifu wa mgodi wa chuma pamoja na usanifu wa kiwanda cha chuma - Liganga, na kulipa fidia	• Kukamilika kwa ukarabati wa barabara ya Itoni - Mkiu – Liganga na Mchuchuma kwa kiwango cha changarawe; • Kukamilika kwa uthamini wa mali za wananchi watakaopisha eneo la mradi Mchuchuma na Liganga; • Kupatikana kwa leseni za uchimbaji wa makaa ya mawe na chuma;

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		wananchi wanaozunguka eneo la Mchuchuma; na • Kupitia tafiti za athari za mradi kimazingira.	• Kuendelea na mazungumzo kati ya wawekezaji (Tanzania – China Mineral Resources Limited) na TANESCO juu ya mkataba wa kuuza umeme utakaozalishwa Mchuchuma; na • Kupatikana kwa vyeti vya mazingira kwa mradi wa Mchuchuma, mgodi na kiwanda cha chuma Liganga, cheti cha ujenzi wa kituo cha kufua umeme, na cheti cha msongo mkubwa wa umeme kutoka Mchuchuma hadi Liganga.
	Kiwanda cha Viuadudu Kibaha, Pwani	• Kukamilisha ufungaji wa mitambo ya kiwanda, kuanza uzalishaji na kujenga barabara ya kuingilia kiwandani.	• Kukamilika kwa kiwanda na kuanza uzalishaji Julai 2015; na • Ujenzi wa barabara ya kuingilia kiwandani kwa kiwango cha lami umekamilika;
Maendeleo ya Rasilimali Watu	Maendeleo ya Ujuzi Maalum	• Kuendeleza ujuzi katika fani mbalimbali ili kuongeza wataalam ambao watakidhi mahitaji ya Taifa kwa sasa na baadaye hususan katika fani ya mafuta na gesi.	• Kuendelea kupatiwa mafunzo katika fani za mafuta na gesi kwa ngazi mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa wanafunzi 159 ambapo wanafunzi 124 wanagharamiwa na Serikali na wanafunzi 35 wanagharamiwa na nchi wahisani.
	Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Vyuo Vikuu)	• Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; na • Ujenzi wa miundombinu ya vyuo vikuu, vyuo vya ufundi stadi, vyuo vya ualimu, vyuo vya maendeleo ya wananchi na maendeleo ya jamii;	• Shilingi 135,803,000,000 zimetolewa kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ikilinganishwa na lengo la shilingi 246,341,409,579 kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2015/16 ambapo shilingi 134,685,646,257 zimetolewa kwa wanafunzi 119,073; • Kukamilika kwa jengo la umwagiliaji na kusimika mitambo katika maabara ya uhandisi wa umwagiliaji katika Chuo cha Ufundi Arusha; na • Kuendelea na ujenzi wa jengo la hospitali ya kufundishia ghorofa ya 4 katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Dar es Salaam - Kampasi ya Mlonganzila.

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
	Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETC)	• Kuanza ujenzi wa vyuo vya ufundi katika mikoa ya Simiyu, Njombe, Rukwa na Geita.	• Kupata mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika wa Dola za Kimarekani milioni 52.02 kwa ajili ya kujenga vyuo vya ufundi katika mikoa ya Njombe, Simiyu, Geita na Rukwa. Sehemu ya fedha itatumika kupanua na kuimarisha vyuo vya Ualimu vya Dakawa, Tabora, Marangu, Butimba, Mpwapwa na Kleruu - Iringa na kuviunganisha vyuo hivyo katika mkongo wa Mawasiliano wa Taifa na Kuvipatia vyuo hivyo sita vya ualimu vifaa na kemikali ili kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa walimu tarajali.(toa)
	Elimu ya Msingi na Sekondari	• Kusambaza vitabu, kuimaraisha ukaguzi wa shule na kutoa mafunzo ya kusoma, kuandika na kuhesabu kwa walimu na wanafunzi,.	• Kutoa mafunzo kwa walimu 630 katika Halmashauri 40 nchini; • Kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya madarasa, vyoo, maabara na nyumba za walimu katika shule za msingi 528; na • Kupatiwa mafunzo kwa walimu 5,868 wa masomo ya Sayansi, Hisabati, Biolojia na Lugha.
	Afya na Ustawi wa Jamii	• Kuboresha utoaji wa huduma katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili; • Kuendeleza awamu ya tatu ya ujenzi wa Taasisi ya Mifupa MOI; • Ununuzi wa vifaa tiba na kuanza ujenzi wa jengo la Taasisi ya Saratani Ocean Road; • Kuimarisha hospitali za rufaa na hospitali za magonjwa maalum za Mbeya, Mtwara, Bugando, Kibong'oto, Mirembe na KCMC;	• Hospitali ya Taifa Muhimbili: kuendelea na ujenzi wa jengo la dharura kwa watoto; • Kituo cha Tiba na Mafunzo ya Upasuaji wa Moyo: Ununuzi wa vifaa tiba na kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kibingwa; • Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI): kukamilika kwa ujenzi wa jengo la ghorofa 7 litakalokuwa na sehemu za kutolea huduma pamoja na malazi kwa wagonjwa; • Taasisi ya Saratani Ocean Road: kuanza ujenzi wa vyumba maalum (*bunkers)* kwa ajili ya kusimika mashine za kisasa kwa ajili ya kutolea tiba ya mionzi;

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
		• Usimamizi na kupunguza vifo vya wajawazito nchini; • Mpango wa kudhibiti kifua kikuu na ukoma; na Mpango wa Kudhibiti UKIMWI na ununuzi wa dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI kwa waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI.	• Hospitali za Rufaa za Kikanda: Kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa kanda ya kati iliyopo Singida; kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la tiba ya mionzi katika Hospitali ya Bugando; ukarabati wa wodi 6 katika hospitali ya Kibong'oto; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la *X-rays* katika hospitali ya Rufaa ya Mbeya; kuanza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje la hospitali ya Kanda ya Kusini-Mtwara; na • Ujenzi wa hospitali ya kisasa Benjamin Mkapa Ultra Modern Hospita**l** - Dodoma umekamilika. Hospitali itatumika kwa tafiti na kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa afya katika Chuo Kikuu Dodoma.
Huduma za Utalii, Biashara na Fedha	Utalii	• Ujenzi wa kitega uchumi cha Utalii House awamu ya pili katika eneo la ubalozi wa zamani wa Marekani; na • Kuboresha huduma za utalii ili kuvutia watalii wengi zaidi na kuongeza mapato yatokanayo na utalii.	• Kuendelea na usanifu wa ujenzi wa Utalii House awamu ya pili; • Uboreshaji wa mfumo wa ukusanyaji mapato ya utalii, uwindaji na upigaji picha; • Kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka nje kutoka watalii 1,095,884 mwaka 2013 hadi watalii 1,140,156 mwaka 2014; na • Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii kutoka dola za Kimarekani bilioni 1.86 mwaka 2013 hadi dola za Kimarekani bilioni 2.01 mwaka 2014.
	Biashara na Masoko	• Kupitia Sheria Na. 10 ya mwaka 2005 ya mfumo wa stakabadhi za ghala ili iweze kuendana na soko la mazao na bidhaa litakaloanzishwa.	• Kurekebishwa na kupitishwa bungeni kwa sheria ya mfumo wa stakabadhi za ghala; na • Kuanzishwa kwa kampuni ya kusimamia na kuendesha soko la mazao ya bidhaa ijulikanayo kama *Tanzania Mechantile Exchange (Public Limited Company)*.
	Ushirikiano wa	• Kukamilisha ujenzi wa vituo vya utoaji	• Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya utoaji huduma za pamoja

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
	Kikanda na Kimataifa	huduma za pamoja mipakani; na • Kujenga, kukarabati na kununua majengo ya Balozi.	mipakani vya Sirari/Isebania, Holili/Taveta, Horohoro/Lungalunga na Namanga (Tanzania/Kenya), Mtukula/Mutukula (Tanzania na Uganda), Rusumo (Tanzania na Rwanda); • Ujenzi wa kituo cha Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi) umefikia asilimia 85; • Ujenzi wa kituo cha Songwe/Kasumulu (Tanzania na Malawi) upo katika hatua za mwisho za kumpata mkandarasi kwa ajili ya usanifu; • Ununuzi wa majengo 2 jijini Paris - Ufaransa kwa ajili ya ofisi na makazi ya Balozi; na • Ukarabati wa jengo la Ofisi za Ubalozi Jijini New York na Maputo unaendelea.
Huduma za Fedha	Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania	• Kuongeza mtaji na kuanza kutoa huduma.	• Mtaji wa benki ni shilingi bilioni 60; na • Kuidhinishwa kwa kanuni na muundo wa utumishi, kanuni za fedha na kuendelea kwa taratibu za kukamilisha masharti ya upatikanaji wa leseni ya kudumu ya shughuli za kibenki.
	Benki ya Rasilimali Tanzania	• Kuongeza mtaji na kuimarisha huduma za kibenki hususan utoaji wa mikopo pamoja na mafunzo kwa wajasiriamali.	• Mtaji wa benki umefikia shilingi 152,137,661,000; na • Mikopo iliyotolewa ni shilingi 413,044,192,000 katika sekta za kilimo, uwekezaji wa ardhi na majengo, viwanda, utalii, misitu, biashara, uchimbaji madini, mafuta na gesi, ujenzi, usafirishaji na mawasiliano, elimu na afya, hoteli na migahawa.
	Benki ya Maendeleo ya Wanawake Tanzania	• Kuongeza mtaji na kuimarisha huduma za kibenki hususan utoaji wa mikopo na mafunzo kwa wajasiriamali	• Mali za benki zimefikia shilingi bilioni 34.8; na • Kuongezeka kwa amana za wateja kufikia shilingi bilioni 26.6.
	Vikundi vya	• Utekelezaji wa programu za	• Kusajili vikundi vya SACCOS 5,559 na kufikisha wanachama

SEKTA	MRADI	MALENGO	UTEKELEZAJI
	Wajasiriamali Wadogo	kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia urasimishaji wa biashara za wajasiriamali wadogo na maendeleo ya SACCOS na VICOBA.	1,153,248 waliojiunga na kunufaika; • Kuongezeka kwa mikopo inayotolewa na SACCOS kwa wanachama hadi kufikia shilingi bilioni 893; na • Kuanzishwa kwa VICOBA 23,000 vyenye wanachama 700,000 na mtaji wa shilingi bilioni 86.

Kiambatisho II

Ratiba ya Uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2016/17

Shughuli	Muda	Mhusika
Kuandaa rasimu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17	Septemba - Novemba 2015	Wizara ya Fedha na Mipango
Maoni ya wadau ya rasimu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17	Oktoba, 2015	Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika/ Taasisi, Wakala wa Serikali na Sekta Binafsi
Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/16	Septemba na Desemba 2015 Machi na Juni 2016	Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika/ Taasisi, Wakala wa Serikali na Sekta Binafsi
Kuwasilisha rasimu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17 katika Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bajeti na Bunge	Januari, 2016	Wizara ya Fedha na Mipango na Bunge
Kuandaa rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17	Februari - Mei 2016	Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika/ Taasisi, Wakala wa Serikali na Sekta Binafsi
Uchambuzi wa bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/17	Februari – Machi, 2016	Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika/ Taasisi, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri
Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 na Hali ya Uchumi 2015 katika Kamati ya Kudumu ya Bajeti na Bunge	Mei – Juni 2016	Wizara ya Fedha na Mipango